**Utulivu** watawala uchaguzi mdogo wa Muhambwe na Buhigwe

UKURASA 4



**Wakala** wa vipimo wawaita wenye wasiwasi, mita za maji, umeme kutoa taarifa

UKURASA 8




**Vardy ataja mataji zaidi baada ya FA**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatatu Mei 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580583

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Mwinyi: Tuliwapa wazungu mazao watupatie baiskeli

• **Akumbusha** uhaba wa mafuta ulivyomtesa, mishahara kutopandishwa... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**
**KIKWETE MGENI RASMI MJADALA UBORA WA ELIMU**
RAIS mstaafu wa serikali awamu ya nne, Jakaya Kikwete, anatarajiwa...

**UKURASA WA 3**
**UFINYU WA BAJETI WAATHIRI UTEKELEZAJI MIRADI YA AFYA**
KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imesema...

**UKURASA WA 4**
**WAZIRI LUKUVI AWAFUNGULIA MILANGO WENYE MALALAMIKO**
WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amejitwisha...


## Nafasi za kina Mdee BAWACHA kuanza kujazwa

UKURASA 3



Watoto wakicheza michezo mbalimbali iliyoandaliwa katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, kusherehekea Sikukuu ya Eid el Fitri mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Anglikana kurejeshewa maeneo yaliyovamiwa

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA: TUTAPINDUA MEZA KWA MKAPA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mwinyi: Hii ndiyo sababu ya kuwapa mazao 'wazungu' wakatupatia baiskeli

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amekumbusha uhaba wa fedha za kigeni ulivyoikumba Tanzania mwanzoni mwa uongozi wake kiasi cha kufikia hatua ya kubadilishana bidhaa kwa bidhaa na nchi za Ulaya na Asia ili kukwepa kutumia fedha za kigeni.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema hali hiyo mbaya kiuchumi ikisababishwa na masharti magumu yaliyotolewa na Benki ya Dunia, IMF na wakopeshaji wengine dhidi ya Tanzania na hasa uamuzi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kuifukuza timu ya IMF.

Anayataja baadhi ya masharti yaliyowekwa kuwa ni IMF kutaka thamani ya Shilingi ya Tanzania ipunguzwe kwa asilimia 25, kupandisha riba za benki, kupunguza matumizi ya serikali, kusitisha nyongeza ya mishahara, kuondosha udhibiti wa bei na kulegeza udhibiti wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Anasema kutokana na mvutano huo, uzalishaji uliohitaji kuagiza malighafi, vipuri na mafuta kutoka nje ukaathirika, huku TAZARA ikisimamisha huduma Aprili 1982.

"Wauzaji kutoka nje wakadai walipwe kabla ya bidhaa hazijasafirishwa kuja Tanzania. Meli za mafuta zikakataa kupakua mafuta bandarini mpaka walipwe kwanza, na wakati mwingine zilikaa bandarini Dar es Salaam kwa wiki kadhaa wakisubiri malipo. Ninavyokumbuka, kuna waliokubali walipwe kahawa wakaiuze wenyewe mbele ya safari.

"Tatizo la mafuta lilitusumbua sana. Ikabidi Machi 1980 serikali iongeze bei ya mafuta kwenye bajeti ya mwaka 1980/81. Wenye magari wakaruhusiwa kununua petroli kwa siku tatu tu za juma.

"Ofisi za kibalozi na maofisa wa balozi wakatakiwa kununua petroli kwa fedha za kigeni. Serikali ikajitahidi kuzungumza na nchi zinazotuuzia mafuta na zinazozalisha mafuta wanachama wa OPEC kutafuta msaada au unafuu. "OPEC ikatusaidia kidogo, na baadhi ya nchi wazalishaji mafuta zikajitolea kutusaidia kidogo. Algeria, ambayo ilituunga mkono kwenye vita dhidi ya Idd Amin, wakatukopesha Dola milioni 30 kwa riba ya asilimia tatu tu. "Iraq ikatupa mkopo wa masharti nafuu wa Dola milioni nane ikiwa ni nyongeza kwa mkopo mwingine wa Dola milioni 30 waliokuwa wametupatia mwaka 1979," anasimulia. "Mwinyi anabainisha kuwa mbinu nyingine iliyotumika kipindi hicho cha uhaba mkubwa wa fedha za kigeni ni kufanya biashara ya kubadilishana bidhaa ili kukwepa kutumia fedha za kigeni.

Anasema kuwa mwaka 1981 Angola ilikubali kuiuzia Tanzania mafuta kwa mkopo wa masharti nafuu na unaolipwa kwa bidhaa badala ya fedha za kigeni.

"Mwaka 1982 tukaingia mkataba na Msumbiji wa kufanya biashara ya kubadilishana bidhaa badala kulipana fedha. Sisi tuliwapa mabati, kakao na majembe na wao wakatupa matairi na tyubu zake, pamoja na vyerehani.

"Mwaka 1993 tukaafikiana na China na Ujerumani Mashariki juu ya biashara ya kubadilishana bidhaa. Makubaliano yakawa Tanzania iwape Wachina saruji, korosho na mbao na wao watupatie malighafi na vipuri. "Kwa Ujerumani Mashariki makubaliano yakawa kwamba sisi tuwape kahawa, pamba, chai na tumbaku na wao watupatie baiskeli 10,000. Kwa hakika, tulijaribu kila mbinu ya kuishi kwenye mazingira ya uhaba mkubwa wa fedha za kigeni.

"Ili kukabiliana na kushuka kwa uzalishaji na tija kwenye sekta ya umma, kwenye sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi mwaka 1980, CCM ilitangaza sera mpya ya tija na kusema kuwa sasa wafanyakazi watalipwa kulingana na matokeo.

"Kwa maana hiyo iwapo kiwanda cha umma kitapata hasara, menejimenti na wafanyakazi hawatakuwa na haki ya kulipwa nyongeza ya mshahara au kupandishwa vyeo, lakini bonasi zitalipwa pale ambapo kiwanda kimeongeza uzalishaji, tija na faida," anakumbusha.

Ili kutekeleza maagizo hayo ya CCM, Mwinyi anasema serikali ilitoa Waraka wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 1981 na kisha ikatunga Sheria ya Baraza la Tija la Taifa.

Anabainisha kuwa pia iliazimiwa wanasayansi au wafanyakazi watakaobuni mbinu za kukuza uchumi watazawadiwa, wakati wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao watachukuliwa hatua.

"Wakati huo huo kufuatia kilio cha wafanyakazi, Mwalimu akatangaza kuwa itatolewa nyongeza ya mshahara ya asilimia 20 kwenye kima cha chini cha mshahara na kufikia Sh. 480 kwa mwezi mijini na Sh. 340 kwa mwezi vijijini," anasimulia.

## JK mgeni rasmi mjadala wa elimu

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS mstaafu wa serikali awamu ya nne, Jakaya Kikwete, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mkutano wa kujadili masuala mbalimbali kwenye sekta ya elimu nchini.

Mkutano huo utakaofanyika kuanzia kesho hadi Alhamisi 20 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMENT), Ochola Wayoga, alisema katika mkutano huo mada 15 zitajadiliwa huku mada kuu ni uwajibikaji wa pamoja katika kugharimia elimu bora nchini.

Alisema katika kujadili namna ya kuboresha elimu, watatumia tafiti mbalimbali za elimu ambazo zimelenga katika kuboresha elimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

"Kila mwaka TENMET huandaa mkutano wa kujadili ubora wa elimu ambao hutoa fursa kwa wadau wa elimu ikiwamo serikali, wanachama wa mtandao, washirika wa maendeleo kujadili hali ya ubora wa elimu kwa nia ya kuboresha utoaji wake," alisema Wayoga.

"Mwaka huu mkutano huo umeandaliwa kwa kuchukua taswira ya kimataifa ili kutoa fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna ya kuweka mikakati ya kuimarisha ubora wa elimu kati ya nchi moja na nyingine na kutoa mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo kwa kutumia matokeo ya tafiti na uzoefu kutoka nchi nyingine."

Wayoga alisema katika kuimarisha ubora wa elimu nchini, kila mtu kwa nafasi yake anatakiwa kuwajibika ipasavyo iwe ni serikali, walimu, wazazi, wadau wa maendeleo na kwamba katika kufanya hivyo ubora wa elimu nchini utakuwa wa kiwango cha juu.

"Ubora wa elimu hauwezi kuletwa na mtu mmoja, hatuwezi kuiachia serikali peke yake na walimu, isipokuwa sisi sote katika kila eneo tunapswa kuwajibika ipasavyo na hapa ndipo tutafikia malengo tunayoyataka," aliasema Wayoga.

"Kwa mfano serikali inapochukua hatua ya kutoa elimu bure kwa watoto wetu, haimaanishi na wewe mzazi au mlezi na sisi wengine wenye uwezo wa kuchangia tusichangie, na ndiyo maana tumekuwa tukishuhudia kwamba pamoja na serikali kujitoa, lakini bado kuna wadau ambao wanajitokeza na kusaidia."

"Wapo wanaochangia madawati, vifaa na michango mingineyo, lengo likiwa ni moja tu la kuhakikisha elimu yetu inakuwa bora."





Maofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wakimsaidia bibi kuelekea kituo cha kupigia kura mjini Kibondo jana, wakati wa uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Muhambwe. Habari Uk. 4. **PICHA: DEO NSOKOLO**

## Anglikana kurejeshewa maeneo

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameahidi kutatua migogoro ya ardhi inayohusisha maeneo ya makanisa kuvamiwa na watu, yakiwamo ya Kanisa la Anglikana Tanzania.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Mwanza wakati wa ibada maalum ya kumsimika Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Victoria Nyanza, Zephania Ntuza.

Aliahidi kutatua migogoro ya maeneo hayo kuvamiwa, kwamba atamtuma Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kushughulikia suala hilo.

Dk. Mpango alisema amesikia suala hilo, kwamba aliomba uongozi wa kanisa hilo kuandika barua rasmi ili kutafuta ufumbuzi kwa taasisi za dini kuvamiwa.

"Hili suala nimesikia na naomba kama kanisa mlilete kwa maandishi ili tuweze kulishughulikia na kulipatia ufumbuzi," alisema Dk. Mpango.

Kuhusu kuwapo kwa migogoro katika makanisa mbalimbali nchini, Dk. Mpango alisema hatua hiyo inawakatisha tamaa waumini na kuwarudisha nyuma kiroho.

Alifafanua kwamba migogoro isiyo na tija kwa makanisa inahatarisha pia amani ya nchi.

Dk. Mpango alisema serikali inapenda kuona taasisi za dini zinaongozwa kwa kufuata taratibu na kanuni walizojiwekea ili kuepuka migogoro mbalimbali.

"Tumechoka kusikia migogoro hiyo, ambayo inakatisha tamaa na kurudisha nyuma waumini kiimani, kuwagawa na kushindwa kutekeleza mambo ya kuwajenga kiroho," alisema Makamu wa Rais.

Kutokana na hilo, Dk. Mpango alisema hatarajii askofu aliyepigiwa kura na kupewa nafasi hiyo kuona anageuka na kuwa mtu mbaya, asiyefuata taratibu, kanuni za kanisa, kutumia vibaya madaraka pamoja na ufujaji wa mali za kanisa.

Alisema kanisa limekuwa mshirika katika utoaji wa huduma za kijamii hususani maeneo ya vijijini, ikiwamo sekta ya maji, elimu, kilimo na afya.

Dk. Mpango alisema serikali itaendelea kushirikiana na kanisa kwa kuweka mazingira mazuri, ili waweze kuwahudumia wananchi ipasavyo na kuongoza wigo la utoaji huduma za kiroho.

Naye Askofu Ntuza alisema atahakikisha anasimamia haki kwa waumini wote na kutii katiba na kanuni ya kanisa hilo ili kuendeleza mshikamano.

Aliongeza kuwa amekubali kufungwa na sheria na kanuni zote zilizowekwa na zitakazowekwa tangu sasa na kanisa hilo na kuangalia misingi, sheria na masharti ya dayosisi hiyo.

Aidha, aliomba ushirikiano kutoka kwa viongozi na waumini wa dayosisi hiyo, ili kusogeza mbele imani za waumini hao pamoja na kuleta amani, upendo, umoja na mshikamano.

**Imeandikwa na Richard Makore na Neema Emanuel, MWANZA**

## HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula, akitoa maelezo kwenye mkutano wa 11 wa makatibu tawala wa mikoa, makatibu tawala wilaya na wakurugenzi wa wilaya uliofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Nafasi za kina Halima Mdee zaanza kujazwa BAWACHA

**Na Elizabeth Zaya**

NAFASI za uongozi wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) zilizoachwa wazi zinatarajiwa kupatikana kesho kwenye uchaguzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Bara, Benson Kigaila, tayari Kamati Kuu ya CHADEMA iliyokutana Mei 12, mwaka huu ilifanya usaili, kujadili na kuteua wagombea wa nafasi mbalimbali zinazotarajiwa kufanyiwa uchaguzi.

Miongoni mwa nafasi za BAWACHA zitakazofayiwa uchaguzi kesho ni ya Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Uratibu wa Uenezi.

Uchaguzi huo unafanyika baada ya viongozi waliokuwa wakishika nafasi hizo kuvuliwa uanachama Novemba 27, mwaka jana kutokana na kilichoelewa ni kukiuka katiba na kanuni za chama hicho.

Viongozi hao wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Halima Mdee, walikwenda kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum pasipo kupitishwa na chama.

Kwa mujibu wa Kigaila, uchaguzi huo utafanyika jijini Mwanza.

Kwenye taarifa hiyo, Kigaila alisema: "Kamati kuu ya chama iliyokutana Mei 12, mwaka huu ilifanya usaili, kujadili na kuteua wagombea wa nafasi mbalimbali zinazotarajiwa kufanyiwa uchaguzi katika Baraza la Wanawake."

Aliongeza: "Kamati Tendaji ya Baraza itakutana jijini Mwanza Mei, 18 kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa viongozi hao kwa mujibu wa mwongozo wa baraza hilo kifungu cha 7.8.5(a)(b)(c)(d)."

Wanaowania nafasi ya Katibu Mkuu ni Aisia Msangi, Catherine Ruge na Esther Daffi.

Nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Bara ni Brenda Jonas, Emma Boki na Nuru Ndosi wakati anayewania nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Zanzibar ni Bahati Haji.

Wanaowania nafasi ya Uratibu na Uenezi ni Aisha Ame, Husna Said na Sigrada Mlingo.

Akizungumza na Nipashe jana kutoa ufafanuzi wa nafasi ya mwenyekiti kutokuhusishwa katika uchaguzi huo, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje, John Mrema, alisema nafasi ya mwenyekiti itaendelea kukaimiwa hadi mkutano mkuu wa baraza hilo, utakapokutana na kufanya uchaguzi.

Mrema alisema: "Kwa mujibu wa katiba, Mkutano Mkuu wa BAWACHA ndiyo wenye mamlaka ya kutoa jina la Mwenyekiti, kwa hiyo Kamati Tendaji itaamua aidha nafasi hiyo iendelee kukaimiwa au kuitishwe mkutano mkuu kwa ajili ya kumchagua mwenyekiti mwingine."

# Ufinyu wa bajeti wakwamisha miradi ya afya

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imesema kuwa upatikanaji mdogo wa fedha za maendeleo umeathiri miradi ya kipaumbele iliyoidhinishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020/21.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti Stanslaus Nyongo, alisema athari hizo ni pamoja na upatikanaji wa dawa, kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi na kudhibiti Ukimwi.

Alisema kuwa hadi Machi 2021, wizara ilipokea jumla ya Sh. 409,018,849,518.72 sawa na asilimia 45.4 ya fedha zote zilizoidhinishwa ikiwa ni kwa ajili ya mishahara, matumizi mengine huku miradi ya maendeleo ikiambilia asilimia 23 pekee.

"Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa kati ya fedha za ndani zaidi ya Sh. bilioni 76.5 sawa na asilimia 27.25 ya lengo, fedha za nje ni Sh. bilioni 6.6 sawa na asilimia 8.29 ya lengo," alisema.

Kwa mujibu wa Nyongo, Wizara ya Afya iliidhinishiwa zaidi ya Sh. bilioni 900 na kati yake Sh. bilioni 539.1 sawa na asilimia 59.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 360.9 sawa na asilimia 40.1 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kuhusu suala la Bima ya Afya kwa wote limekuwa agenda ya Bunge kwa muda mrefu kupitia kamati hiyo, lakini halijatekelezwa na mara zote wameambiwa kuwa mchakato unaendelea.

"Kamati ilihoji hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ushauri huu na ilielezwa kuwa serikali itahakikisha inaleta muswada katika mkutano wa tatu wa bajeti na tayari Sh. milioni 231 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya kutungwa kwa sheria ya Bima ya Afya kwa wote na utoaji wa elimu kwa umma," alisema.

Nyogo alisema kamati hiyo inaamini kuwa muswada utaletwa kama ilivyoahidiwa ili kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya nchini.

Alisema, kamati hiyo ilishauri wananchi na sekta binafsi kushirikishwa vya kutosha ili kutoa maoni yao katika kuboresha muswada.

Pia Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, akijibu hoja mbalimbali alisema serikali itashirikisha wadau wote muhimu katika muswada huo, huku akiahidi kutatua suala la ukosefu wa dawa kwa wanaotumia bima ya afya.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 26 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SILVESTER BAKARI SWAI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**AURERIA SWAI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitsho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 8 mwezi wa JUNE mwaka 2021

**Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 6th mwezi MAY 2021**

NAIBU MSAJILI

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 46 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUZA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**NGUSA JULIUS NDEMA**
**MWOMBAJI/ WAOMBAJI**
**REGINA WASHEKU MONDEYA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16th Mwezi wa June, 2021.

**Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 11th Mwezi wa May, 2021**

NAIBU MSAJILI

NHC
TUNAJENGA TAIFA LETU

**TANGAZO KWA WAPANGAJI MKOA WA DAR ES SALAAM**

1. Tunapenda kuwafahamisha wapangaji wetu waliopo Mkoa wa Dar es Salaam kuwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limeanzisha Mkoa mpya wa Dar es Salaam Metropolitan. Uamuzi huu wa Shirika unalenga kusogeza huduma zetu za upangaji kwa wateja wetu.
2. Mkoa huu wa Dar es Salaam Metropolitan umetokana na kumegwa maeneo yaliyokuwa katika Mikoa yetu ya Upanga na Ilala.
3. Maeneo yanayounda Mkoa huu mpya wa NHC yanahusisha majengo yote yaliyopo katikati ya mitaa ya Azikiwe upande wa Mashariki, Mtaa wa Mosque upande wa Magharibi, Barabara ya Sokoine upande wa Kusini na Bibi Titi Mohamed upande wa Kaskazini.
4. Tunawaomba wateja wetu wanaopanga na kuishi katika maeneo hayo, wafahamu kwamba kuanzia tarehe 1 Juni 2021 watakuwa wanahudumiwa na Mkoa huo mpya. Ofisi za Mkoa huu zipo katika jengo la Diplomat kiwanja Na. 26 kwenye makutano ya Barabara ya Mkwepu na Kaluta ghorofa ya sita.
5. Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linaahidi kuwa litaendelea kuwapa wapangaji wa Mkoa huu mpya huduma bora za upangaji kama ilivyokuwa katika mikoa yao ya awali.

**LIMETOLEWA NA:**
**KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**
**MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA | SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000**
**BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com**

# Waziri Lukuvi awafungulia milango wenye malalamiko

Na Munir Shemweta

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amejitwisha mzigo wa kuwasaidia wananchi wenye malalamiko ya kulipwa fidia kwenye maeneo mbalimbali.

Waziri Lukuvi ameanza utaratibu huo kupitia mpango maalumu aliouanzisha uitwao 'Funguka kwa Waziri' kwa kuamua kuchukua hatua ya kuandika barua za madai kwa taasisi na idara zinazodaiwa fidia.

Amelazimka kuanzisha utaratibu huo baada ya wananchi waliotoa maeneo yao kwa shughuli mbalimbali za maendeleo, kuamua kuwasilisha malalamiko kwake kupitia fomu maalum za Funguka kwa Waziri.

Akizungumza katika kipindi Maalum cha Funguka kwa Waziri kilichorushwa na mojawapo ya kituo cha televisheni, Waziri Lukuvi alisema, uchambuzi wa malalamiko na migogoro ya matumizi ya ardhi yaliyowasilishwa kwake ulionesha malalamiko mengi yapo kwenye masuala ya fidia.

Alisema katika uchambuzi huo asilimia 39.4 ya malalamiko yako katika masuala ya fidia, huku uvamizi wa maeneo ukiwa na asilimia 29.4, migogoro ya kifamilia asilimia 22.9, iliyopo mahakamani ni asilimia 5.5 na malalamiko ya milki na upimaji pandikizi ikiwa ni asilimia 2.8.

"Rais alishatoa maelekezo wote waliochukua ardhi ya wananchi lazima walipwe fidia, wote waliorudisha fomu za Funguka kwa Waziri kwangu mimi nimechukua uwakili na nitaandika barua kwa kila anayedaiwa fidia iwe Mkurugenzi, Katibu Mkuu au Mkurugenzi wa TANROAD,'' alisema Lukuvi.

Alisema, hadi kufikia Aprili 30, mwaka huu fomu zilizochukuliwa na wananchi zilikuwa 24,442, kwamba fomu zilizojazwa ni 3,171, malalamiko yaliyofanyiwa kazi ni 1,144.



Mshauri Mwelekezi wa Haki Elimu kutoka Asasi za kiraia, Dk. Wilberforce Meena, akitoa mafunzo ya elimu jumuishi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum washiriki kwenye warsha hiyo, wakiwamo wadau wa elimu, baraza la utetezi wa watoto na kikundi cha wazazi iliyofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Utulivu watawala uchaguzi mdogo Muhambwe, Buhigwe

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

HALI ya utulivu na amani imetawala katika uchaguzi mdogo wa ubunge majimbo ya Muhambwe wilayani Kibondo na Buhigwe, huku idadi ndogo ya wapigakura ikijitokeza kupiga kura katika vituo mbalimbali.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza mapema kupiga kura walisema hakukuwa na pingamizi lolote walilopata wakati wa uchaguzi huo.

"Nilijua nitakuta foleni kubwa, lakini hali ni tofauti, nimefika hapa na kupiga kura yangu bila shida yoyote na kwa haraka," alisema Isabela Kabululu.

Winfrida Lulimbie, kwa upande wake alisema pamoja na kuumwa, uchaguzi huo ni muhimu zaidi kwake kwa kuwa anahitaji kupata kiongozi ambaye atasaidia kuleta maendeleo katika wilaya hiyo.

Alisema alilazimika kuwaomba wajukuu zake wambebe ili atimize haki yake ya kupiga kura katika uchaguzi huo kwa kuwa anaamini hiyo ndio fursa pekee ya kuweka kiongozi unayemtaka.

Mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Florence Samizi, alisema ana imani ataibuka na ushindi kwa kuwa alifanya kampeni katika maeneo yote na ilani ya uchaguzi ya chama chake inatekelezeka.

Pia alisema ameridhishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilivyoratibu uchaguzi huo kwa kuwa kila kitu kimekwenda vizuri na watu wote wamepata fursa ya kupiga kura.

Mgombea wa Chama cha ACT-Wazalendo, Julius Masabo, alisema ameridhishwa na uchaguzi kwa kuwa alihakikisha kila kituo kina vifaa na wakala wake na wamekuwa wakishirikishwa kikamilifu na msimamizi wa uchaguzi katika zoezi zima.

Alisema maandalizi mazuri yaliyofanywa na Tume yanatoa ishara ya wananchi kuheshimiwa katika maamuzi watakayofanya kupitia karatasi ya kura.

Msimamizi wa uchaguzi katika Jimbo la Muhambwe, Diocles Lutema, alisema zaidi ya wapigakura 127,000 walitarajiwa kupiga kura katika uchaguzi huo kwenye vituo 336.

Alisema wanatarajia kutangaza matokeo mapema kwa kuwa nafasi inayogombewa ni moja na wameweka vituo vingi ili kuwe na urahisi wa kupiga kura na ukusanyaji matokeo na kwamba vifaa na taratibu zote zilifanyika kwa wakati katika vituo vyote.

Alifafanua kuwa, wingi wa vituo ndio unafanya watu kuonekana wachache katika vituo kwa kuwa wanapiga kura na kuondoka.

Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, Luis Bura, alisema serikali imeimarisha ulinzi katika maeneo yote ili kuhakikisha uchaguzi mdogo huo unafanyika kwa amani na utulivu.

Uchaguzi mdogo katika Jimbo la Muhambwe, wilayani Kibondo unafanyika kufuatia kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo marehemu Atashasta Nditiye, aliyefariki mapema mwaka huu jijini Dodoma kwa ajali ya gari.

Vyama vya CCM, ACT-Wazalendo na Democratic Party (DP), vimesimamisha wagombea katika uchaguzi huo.

**BUHIGWE**

Idadi ya wapiga kura waliojitokeza kupiga kura katika Jimbo la Buhigwe kwenye uchaguzi mdogo, imeonekana kuwa ndogo jana asubuhi kwa kinachodaiwa baadhi ya watu kwenda kwenye nyumba za ibada.Jumla ya wapiga kura 112,333, walitarajiwa kupiga kura kumchagua mbunge wa Jimbo la Buhigwe, huku vyama 13 vya siasa vikisimamisha wagombea katika uchaguzi huo. Vyama hivyo ni pamoja na CCM (Eliadory Kavejuru), ACT- Wazalendo (Kudra Garula), AAFP (Balltazary Bianna), ADA TADEA (Mponda Amani), ADC (Mariam Salum), CCK (Rehema Soa), CHAUMMA (Abdalah Bukuku), Demokrasia Makini (Mohammed Msanya), NLD (Rebecca Mwita), SAU (Yunus Masenga), UDP (Anna Peter), UMD (Safia Hussein) na UPDP (Finias Lwitakubi).

Mkazi wa kijiji cha Buhigwe, Ntahu Rubanguka, alisema siku ya Jumapili ni ya kusali na wapiga kura wengi walienda kanisani kabla ya kwenda kupiga kura.

Uchaguzi huo umefanyika baada ya aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Dk. Philip Mpango, kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais.

Msimamamizi wa uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Buhigwe, Marrycelina Mbehoma, amesema zoezi la upigaji kura linaendelea vizuri katika vituo vyote. Alisema katika jimbo hilo kuna vituo vya kupigia kura 290 na mpaka sasa hakuna changamoto yoyote iliyojitokeza ya kukwamisha shughuli.

# Wadau waombwa kusaidia uboreshaji vyuo vya ufundi

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ametoa wito kwa wadau wa maendeleo kusaidia kuboresha miundombinu katika vyuo vya ufundi vya watu wenye ulemavu ambavyo vipo katika kanda zote.

Ametoa wito huo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki alipokuwa akipokea mabweni mawili katika Chuo cha Ufundi Stadi kwa watu wenye ulemavu cha Yombo ambayo yamefanyiwa ukarabati na Shirika lisilo la kiserikali la Nyota Foundation kwa gharama ya Sh. milioni 80.

"Serikali tumejitahidi sana kuboresha vyuo hivi, lakini niwaombe wadau wengine, kampuni, taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa waviangalie sana vyuo vyetu. Vyuo hivi vinakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu pamoja na upungufu wa miundombinu muhimu vikiwamo vyoo, madarasa, mabweni na miundombinu nyinginezo," alisema Mhagama.

Kwa mujibu wa Waziri Mhagama, kwa takwimu za mwaka 2019/2020, Tanzania ilikuwa na jumla ya watu milioni 55.9; Kati ya idadi hiyo, watu milioni 2.5 ni wenye ulemavu na hivyo kuongeza mahitaji ya huduma na miundombinu kwa ajili ya kundi hilo.

Awali, akimkaribisha Waziri Mhagama katika hafla hiyo, Naibu wake anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, alimpongeza kwa kujitoa kwake katika kuboresha mazingira na hali za watu wenye ulemavu kupitia kuwashirikisha wadau wa maendeleo.

Mwakilishi wa Shirika la Nyota Foundation, Zainab Mvungi, alishukuru serikali kwa kuruhusu ukarabati huo kufanyika pamoja na kutoa ushirikiano wakati wote walipokuwa wakifanya kazi hiyo.

Chuo cha Ufundi Stadi Yombo kinachomilikiwa na serikali, kilianzishwa mwaka 1973. Chuo hicho ambacho ni kwa ajili ya Kanda ya Mashariki ni miongoni mwa vyuo sita ambavyo vipo katika kanda mbalimbali kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ufundi kwa vijana wenye ulemavu nchini. Vyuo vingine vipo Kanda ya Kusini (Mtwara), Magharibi (Tabora), Ziwa (Mwanza), Kaskazini (Tanga) na Kati (Singida).

TRA

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## HAKI NA WAJIBU WA MLIPAKODI

### HAKI

1. Kusikilizwa na Kuhudumiwa bila upendeleo
2. Kupewa fursa ya kuaminiwa
3. Haki ya kuwasilisha malalamiko au pingamizi la makadirio
4. Kutatuliwa malalamiko na kupewa majibu ya maulizo yako kwa wakati

### WAJIBU

1. Kulipa kodi au ushuru kabla au mnamo tarehe ya mwisho ya kulipa kodi husika
2. Kutuma ritani za kodi katika kipindi kilichowekwa kisheria
3. Kutunza kumbukumbu za biashara, kutoa na kudai risiti katika mauzo na manunuzi
4. Kutoa taarifa za maandishi TRA pindi unapofunga biashara yako

Kwa maelezo zaidi, piga simu bure; 0800-780078 au 0800-750075,
WhatsApp: 0744-233 333 Barua pepe: huduma@tra.go.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba ikijipanga inaweza kuitoa Kaizer Chiefs J'mosi

**HATIMAYE** wawakilishi pekee wa Tanzania, Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wameanza vibaya mkondo wa kwanza wa robo fainali baada ya kukubali kipigo cha mabao 4-0 ugenini dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Simba ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kushinda mchezo huo na kurahisisha kazi ya kusonga mbele kutokana na rekodi yake nzuri kwenye michuano hiyo msimu huu baada ya kuongoza kwenye msimamo wa Kundi A lililokuwa likijumuisha mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly ya Misri, timu ngumu na zoefu ya AS Vita ya DR Congo na vigogo Al-Merrikh ya Sudan.

Hiyo ni kutokana na Simba kumaliza ikiwa na pointi 13 baada ya kushinda mechi nne, sare moja na kupoteza mchezo mmoja tu ugenini dhidi ya Al Ahly ikiwa ni baada ya kuwanyuka mabingwa hao watetezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku ikipata matokeo nyumbani na ugenini dhidi ya AS Vita na kisha kuichapa Al-Merrikh hapa nchini.

Wengi waliidharua Kaizer Chiefs iliyokuwa Kundi C, kutokana na kumaliza nafasi ya pili kwa faida ya 'head to head' (matokeo ilipokutana) na Horoya FC ya Guinea baada ya timu hizo kila moja kuhitimisha msimamo wa kundi ikiwa na pointi tisa kutokana na kushinda mechi mbili, sare tatu na kupoteza mchezo mmoja, huku Wydad Casablanca ya Morocco ikimaliza kinara na Petro de Luanda ya Angola ikiburuza mkia.

Hata hivyo, kama inavyofahamika kwamba mpira wa miguu una matokeo matatu; kushinda, kupoteza na sare, mashabiki, viongozi, wapenzi wa soka nchini, wachezaji na benchi la ufundi la klabu ya Simba, hawana budi kupokea kipigo hicho na timu kuanza kujipanga kuelekea mechi ya marudiano.

Timu hizo zitarudiana Jumamosi wiki hii na mshindi wa jumla, ndiye atakayetinga nusu fainali ya michuano hiyo, hivyo kilichotokea juzi ni dakika 90 za kwanza tu kati ya 180 ambazo zitakamilikia Uwanja wa Benjamin Mkaka, Dar es Salaam.

Tunaamini kama Simba itafanya maandalizi ya kutosha huku mashabiki na Watazania kwa ujumla wakiwa nyuma yao katika mechi hiyo, hakuna kinachoshindikana kwa kuwa hii haitakuwa mara yao ya kwanza kupindua matokeo.

Ingawa hatuwezi kuishi kwa historia, lakini tukikumbuka maajabu Simba iliyoyafanya ugenini mwaka 1979 kwenye michuano hiyo baada ya kuangukia kipigo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Mufulira Wanderers FC ya Zambia na kwenda kupindua matokeo ugenini kwa kushinda 5-0, hilo linatosha kuamini inawezekana kwa Wekundu wa Msimbazi hao. Lakini pia, Simba inafahamika kwa ubora wake inapokuwa uwanja wa nyumbani, ambao imeugeuza kama 'machinjio' kwa wageni wanapokutana nao katika dimba hilo la Mkapa, hivyo haitakuwa ajabu kuiona ikipindua matokeo na kusonga mbele.

Jambo lingine ambalo linatufanya Nipashe kuamini kwamba inawezekana kwa Simba kupindua matokeo, ni faida ya kuwa na mchezaji wa 12 uwanjani, yaani kucheza mbele ya mashabiki wao kutokana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuruhusu mashabiki 10,000 kuhudhuria mchezo huo tofauti na Kaizer Chiefs ambao walizuiwa kwa sababu ya tishio kubwa la maambukizo ya virusi vya corona nchini kwao.

Kadhalika, ukiangalia kiwango cha Simba ilichokionyesha, nikikubwa zaidi ya wapinzani wao, kutokana na kumiliki mpira kwa asilimia 65 huku umiliki wa Kaizer Chiefs ukiwa asilimia 35, hivyo kilichokosekana ni kukosa umakini kwa washambuliaji na mabeki kufanya makosa. Hivyo, ni wazi Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, na wasaidizi wake watakuwa wameona makosa hayo ya kiufundi katika kikosi chao, hivyo kuelekeza nguvu katika kuyafanyia kazi ili kuweza kupata matokeo chanya Jumamosi.

Kikubwa ni wachezaji kutambua umuhimu wa kupigana kufa au kupona katika dakika 90 za mwisho katika Uwanja wa Mkapa Jumamosi, lakini mashabiki, benchi la ufundi na viongozi kila mmoja kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Hiki ndicho kilichoipoteza Simba kwa Kaizer Chiefs

Na Adam Fungamwango

**KIPIGO** cha mabao 4-0 ilichokipata Simba dhidi ya Kaizer Chiefs kwenye Uwanja wa FNB nchini Afrika Kusini Jumamosi, kimezua maswali mengi kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo, wengine wakiwa hawaamini kilichotokea.

Wakati droo ya michuano hiyo ikitoka, wengi waliamini kuwa Simba imepata mchekea. Ni kwa sababu timu zote ambazo ilibidi zicheze nayo ni za Afrika Kaskazini kwa Waarabu, timu ambazo zinaogopwa sana na mashabiki wa soka hasa wa Afrika Mashariki.

Waliona ni bora kucheza na Kaizer Chiefs kuliko MC Alger au CR Belouizdad za Algeria.

Imekuwa sivyo. Ni kwamba Simba ilikutana na timu yenye wachezaji wenye miili mikubwa, wenye nguvu na kasi pia. Wengi wanajiuliza ni kwa nini Simba ilipoteza mechi hiyo, licha ya kwamba ilimiliki mpira kwa asilimia kubwa?

Kwanza kabisa ni kwamba Simba imekuwa na mfumo mmoja tu wa uchezaji ambao ni wa pasi fupi fupi. Pia wanacheza taratibu, kitu ambacho kinaonekana Kocha Mkuu wa Kaizer Chiefs, Gavin Hunt amekifanyia kazi.

Alichofanya ni kuwaambia wachezaji wake wawaache wapinzani wao wachezee mpira, lakini wao wakiupata wahakikishe wanahama upesi kwenda kushambulia kwa kasi, wakitumia mpira mirefu. Hata baada ya kudhibitiwa kwa staili hiyo, bado Simba haikubadilika na badala yake ilicheza kama ilivyozoea.

Pamoja ya kwamba kuna wakati ndani ya uwanja kulikuwa na mastraika watatu, Chris Mugalu, Meddie Kagere na John Bocco, bado mabeki na mawinga wa Simba walishindwa kucheza mipira mirefu na kupiga krosi, badala yake walitumia muda mwingi kupasiana.

Pili ni kutocheza mipira ya juu. Ni ugonjwa ambao umejirudia kwenye mechi hiyo. Msimu wa 2019 Simba ilikuwa na tatizo la kutocheza mipira ya juu, kushindwa kuokoa mipira ya krosi na faulo, si kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika tu, bali hata Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msimu huu lilionekana kurekebishika hasa baada ya ujio wa beki Joash Onyango ambaye moja ya umahiri wake ni kucheza mipira ya juu.

Aliambukiza na mabeki aliouwakuta, kina Paschal Wawa, Kennedy Juma, Erasto Nyoni na wengineo kiasi kwamba msimu huu, Simba haikuwa na tatizo la mipira ya juu. Cha kushangaza kwenye mechi ya Jumamosi tatizo hilo lilijirudia, tena kwa kiwango cha hali ya juu.

Haijulikani mabeki wa Simba walipatwa na nini, lakini walishindwa kabisa kuruka mipira ya vichwa, kiasi cha kusababisha kufungwa mabao matatu yaliyotokana na uzembe huo.

Tatizo la tatu ni baadhi ya wachezaji kutokuwa kwenye viwango vya kawaida. Wachezaji hao ni Shomari Kapombe na Jonas Mkude.

Pamoja na Mohamed Hussein 'Tshabalala' au 'Zimbwe Jr' kutoa pasi ya kichwa kwa Nurkovic, lakini alicheza vema kwenye mechi hiyo kuliko beki mwenzake wa pembeni Kapombe.

Haijulikani alipatwa na nini. Alionekana kama alitaka kwenda kushambulia, lakini anasita. Akirudi kukaba anachelewa. Kwa kiasi kikubwa ndiye aliyesababisha mabao mawili ambayo timu yake imefungwa kwa kukosa maamuzi ya kukaba kwa kuruka kichwa, au kuokoa.

Wakati mwingine si kwamba alishindwa kuzifikia pasi ambazo alipewa na wachezaji wenzake, hata zile ambazo aliletewa miguuni alishindwa kuzituliza na kutoka nje.

Ni mchezaji aliyeongoza kwa kutokuwa kwenye kiwango chake kilichozoeleka, huku Mkude naye akionekana kushindwa kufanya majukumu yake vizuri.

Kwenye michuano kama hii mikubwa Afrika, nafasi huwa hazipatikani nyingi. Chache tu ambazo zinapatikana zinapaswa kutumika ipasavyo.

Simba ilipata nafasi tatu za wazi ambazo wachezaji Luis Miquissone, Mugalu na Clatous Chama kama wangekuwa makini angalau wangeweza kutumia mbili au moja na kuirahisisha mechi ya marudiano nyumbani Jumamosi.

Kwa hali ilivyo sasa, Simba ina kibarua kigumu kwenye mechi ya marudiano. Lakini kwenye soka lolote linawezekana, ila ni lazima kazi ifanyike. Kwanza ibadili mfumo mzima wa uchezaji ili kuwachanganya wageni ambao wanaonekana wameshawakariri.

Mchezaji kama Bernard Morrison ana umuhimu kwenye mechi hiyo, na akianza pamoja na Miquissone, huku ikiwa na mastraika wawili kati inaweza kuwa msaada mkubwa.

Pia wachezaji waache kuchelewesha mpira kwa pasi fupi fupi zisizo na faida, badala yake kushambulia mfululizo na kupiga mashuti makali ya mbali, kitu ambacho pia kwa sasa Simba ina udhaifu huo.

# Wizara Ujenzi, Mawasiliano, Viwanda kurindima bungeni

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

NI wiki ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuwasilisha bajeti yake ambayo itatoa mwelekeo wa ukamilishaji miradi ya ujenzi wa miundombinu iliyosambaa nchi nzima.

Kwa siku mbili, leo na kesho Bunge litakuwa na kazi ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2021/22, kabla ya kupitisha kwa utekelezaji.

Matarajio ya wengi ni kuona miradi ya ujenzi iliyoanzishwa na awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais Hayati Dk. John Magufuli, inakamilishwa.

Baadhi ya miradi hiyo ni daraja la Selander, daraja la Kigongo Busisi, barabara za juu katika makutano Dar es Salaam, upanuzi wa viwanja vya ndege ikiwamo Uwanja wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma, na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Aidha, katika wiki hii wawakilishi hao wa wananchi watajadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ikiwa ni mara ya kwanza kwa sekta hiyo kuwa na wizara kamili.

Mjadala huo wa siku moja unatarajiwa kujikita katika namna TEHAMA itatumika kuongeza ajira na mawasiliano nchini na jinsi serikali ilivyojipanga kutumia teknolojia kwa kuunganisha na sekta nyingine.

Pia watunga sheria hao watakuwa na kazi ya kujadili kwa siku moja Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo kubwa ni ulinzi na usalama wa mipaka nane ya nchi ambayo Tanzania imepakana na nchi za Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Malawi, Zambia, Congo na Msumbiji.

Wiki hii itamalizika kwa mjadala wa Wizara ya Viwanda na Biashara, ambayo mengi ni uanzishaji wa viwanda na ukuzaji wa biashara ambazo kwa kipindi cha nyuma zilikuwa kwenye misukosuko.

Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani alizionya mamlaka zinazotisha wafanyabiashara, kupokea kodi ya dhuluma ikiwamo kufunga akaunti za wafanyabiashara.

Mjadala unatarajiwa kuangazia ukuaji wa biashara nchini na namna serikali imejipanga kushirikiana na sekta binafsi kukuza na kuendeleza biashara, kwa kuwa sekta hiyo ndiyo injini ya uchumi, idadi ya ajira na kuchangia Pato la Taifa.

# Huduma kidigitali fursa mpya kukuza uchumi

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imeanza kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba matumizi ya huduma za kidijitali yanachangia kukuza uchumi wa kila Mtanzania.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu wiki ya ubunifu ambayo inaanza leo katika mikoa nane ya Tanzania Bara ikiwamo Dar es Salaam.

Dk. Nungu alisema wanaamini kwamba kufikia mwaka 2025 Watanzania asilimia 80 watakuwa wamefikiwa na huduma za kidijitali ikiwamo matumizi ya intaneti.

Alisema miongoni mwa juhudi zinazofanywa na serikali katika kufanikisha lengo hilo ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa kila mwananchi kumiliki simu janja na kwamba kwa kushirikiana na wadau wengine, ina mpango wa kujenga kiwanda cha kutengeneza simu hizo janja ili kuhakikisha kila mtu anaimiliki kwa gharama ndogo.

"Hivi karibuni, serikali iliwaita wadau mbalimbali kujadili namna ya kuimarisha uchumi wa kidijitali nchini na miongoni mwa mipango iliyopo ni pamoja na kuwa na kiwanda cha kutengeneza simu janja ili kumwezesha kila mwananchi kumiliki aina hiyo ya simu ambayo kwa ajili ya kumsaidia kuendesha shughuli zake kupitia intaneti na kukuza uchumu wa kidijitali," alisema Dk. Nungu.

Alisema juhudi nyingine zinazofanywa na serikali katika kufanikisha lengo hilo ni kuunganisha mkongo wa taifa katika maeneo mengi ya nchi ili kila mwananchi atumie intaneti kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF), Joseph Namrakiza, alisema kwa sasa matumizi ya huduma za kidijitali ni muhimu zaidi kwa kuwa yanasaidia kurahisisha kazi katika kila eneo hususani kunapotokea majanga kama ya ugonjwa wa corona.

"Nafikiri kwa sasa kila mtu ameelewa umuhimu wa matumizi ya kidijitali, katika janga kama la corona pasingekuwapo na matumizi ya huduma hizi, ingekuwa vigumu zaidi watu kuendesha shughuli zao, lakini tumeona pamoja na hili janga watu wameendelea na shughuli zao kama kawaida, na ndio maana sisi kama HDIF tunasisitiza kuboresha sekta hii," alisema Namrakiza.

Alisema ikiwa ni mara ya saba kufanyika kwa wiki ya ubunifu nchini, imeleta manufaa makubwa ikiwamo idadi ya wanaoshiriki kuongezeka kutoka 500 kwa Dar es Salaam pekee mwaka 2015 hadi 7,000 kwa mikoa tisa mwaka jana.

"Wiki hii imekuwa ya kitaifa zaidi na imetoa jukwaa kwa wabunifu wengi kuonekana na kuonyesha kazi zao pamoja na kuendelea kujenga mfumo imara wa kuendeleza ubunifu na wabunifu nchini," alisema Namrakiza.

Miongoni mwa wadau walioandaa wiki hiyo ya ubunifu ni HDIF, Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa(UNDP) na COSTECH, huku kaulimbiu mwaka huu ikisema kwamba 'ubunifu kwa uchumi wa kidijitali, stahimilivu na jumuishi.

NMB
Karibu yako

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ILIYOREKEBISHWA

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika kwa njia ya mtandao saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 4, 2021. Kampuni imerekebisha maazimio kwenye Taarifa ya Mkutano Mkuu na imeongeza ajenda nyingine. Kwasasa Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

21.1 MATANGAZO NA AKIDI

21.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

21.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 20 ULIOFANYIKA TAREHE 5 JUNI 2020

21.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 20 WA WANAHISA

21.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

21.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

21.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

21.8 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI

21.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI

21.10 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2021

21.11 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima atume kwa njia ya mtandao nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni (kwa njia ya mkono au mtandao) kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 3 Juni 2021.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya NMB (www.nmbbank.co.tz).
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 137 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 68.5 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2020.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **14 Mei 2021** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **14 Mei 2021** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **2 Juni 2021** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **3 Juni 2021 nakuendelea** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **7 Juni 2021** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa:** | **kuanzia tarehe 16 Juni 2021** |

Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi,

Lilian R. Komwihangiro
Katibu wa Kampuni
7 Mei 2021

www.nmbbank.co.tz

# WMA: Wenye wasiwasi mita za maji, umeme waripoti

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wananchi wenye wasiwasi na mita za maji na umeme kutoa taarifa kwa Wakala wa Vipimo (WMA), ili matatizo yao yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Wito huo ulitolewa jana mkoani Pwani na Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo (pichani) , baada ya kutembelea kituo cha WMA, Misugusugu.

Kituo cha Misugusugu kilichoko Mkoa wa Pwani ni mahsusi kwa ajili ya kuhakiki matangi ya magari yanayobeba vimiminika, mita za maji na umeme.

Alisema amejionea namna matangi ya mafuta yanavyopimwa, mita za maji na umeme na aliwapongeza viongozi wa WMA kwa namna wanavyokitunza.

"Nawapongeza wafanyakazi wa kituo hiki wakiongozwa na Mkurugenzi wao kwa namna wanavyokilinda kituo hiki ambacho ni cha kisasa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati," alisema.

Waziri alisema lengo la WMA ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma zenye vipimo sahihi hivyo wananchi wanaotumia mita za maji na umeme watoe taarifa wanapokuwa na wasiwasi kuhusu usahihi wa mita hizo.

Alisema WMA imesambaa kwenye mikoa yote nchini ili kuwarahishia wananchi wa huko kupata huduma za vipimo wanapoona wanazidishiwa bili.

"Tunajivunia sana kazi kubwa iliyofanyika kukamilisha kituo hiki ambacho ni cha kwanza kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kina vifaa vya kisasa vya kuhakiki mita za maji na umeme," alisema Waziri Mkumbo.



Meneja wa WMA, Mkoa wa Pwani, Alban Kihula, alisema kuanzia kwa sasa wanapima sampuli za mita za umeme, lakini kuanzia wiki ijayo wataanza kuhakiki mita za umeme.

Alisema wataanza kupima mita hizo kuhakiki vipimo vyake kabla ya kuuzwa kwa Shirika la Umeme (TANESCO), ambayo huwafungia wateja mbalimbali nchini.

"Kabla ya kuanza kupima mita za umeme hakukuwa na mtu wa katikati ya TANESCO na mteja anayelalamikia ubora wa mita, lakini sasa hivi mwananchi akiwa na malalamiko anakuja kwetu," alisema.

Alisema hivi sasa hawajaanza kupata malalamiko ya mita za maji wala umeme kwa kuwa ni mara nyingi hupokea malalamiko hayo kutoka kwenye mamlaka husika.

Alisema WMA itaendelea kuhakiki vipimo hivyo ili kuhakikisha mwananchi anapata bili sahihi na mamlaka za maji na TANESCO wanapata malipo stahili.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**

**REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)**

**Date: 17th May, 2021**

***COUNTRY: Tanzania***
***Name of Project*: Resilient Natural Resources for Growth Project (REGROW)**
Loan No. IDA- 61430

Assignment Title: **TENDER NO. TZ-196123-CS- INDV (FIRM SELECTION) PROVISION OF CONSULTANCY SERVICE FOR PRODUCTION OF TOURIST MAP FOR IRINGA TOWN AND RUAHA NATIONAL PARK, IRINGA**

The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the **Resilient Natural Resources for Growth Project (REGROW)**, and intends to apply part of the proceeds for consulting services.

The consulting services ("the Services") includes Provision of Consultancy Service for Production of Tourist Map for Iringa Town and Ruaha National Park, Iringa, purpose of the consultancy is to design, develop a comprehensive tourist map with all important touristic features within the Ruaha National Park and Iringa Municipal. The consultant will be required to gather up-to-date information about all touristic features within the project site and provide suitable design which address all client needs. The results of this work will facilitate tourists to access tourism products and facilities as well as promote tourism attractions within and around the Iringa region and the whole of Ruaha National Park. The contract will be for a period of thirteen (13) weeks.

The Ministry of Natural Resources and Tourism now invites eligible consulting firms (Consultants) to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are the experience in similar assignments; experience in similar conditions; and availability of appropriate skills (Technical and managerial) among permanent staff of the firm.

The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 1.9 of the World Bank's Guidelines: Selection and Employment of Consultants under IBRD Loans and IDA Credits & Grants by World Bank Borrowers of January 2011, revised July, 2014 ("Consultant Guidelines"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.
Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture or a sub consultancy to enhance their qualifications.

A Consultant will be selected in accordance with the Consultant's Qualification Selection (CQS) method set out in the Consultant Guidelines.

Further information can be obtained at the below mentioned address during office hours, i.e. 0900 to 1700 hours, Monday to Friday inclusive, except on public holidays.

Expressions of interest must be delivered in a written form to the Secretary, Ministerial Tender Board, Ministry of Natural Resources and Tourism, located at University of Dodoma, Block 12, Room No L122- Dodoma Monday 31st May,2021 before 10;00 am local time. The envelope shall be clearly marked "Tender No. TZ- 196123-CS- INDV (FIRM) for Provisional of Consultancy Services for Production of Tourist Map for Iringa Town and Ruaha National Park, Iringa for the Resilient Natural Resource Management For Tourism and Growth Project- REGROW.

**Ministry of Natural Resources and Tourism**
**Government City Mtunba,**
**Prime Minister's Street,**
**P.O. BOX 1351**
**40472- DODOMA**
**Tel: +255739173580 /+2557l9173580**
**E-mail: zuwena. zaharan@maliasili.go.tz, regrow@maliasili.go.tz**

# Prof. Mganilwa ataka mfumo rasmi kuwatambua wabunifu

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MKUU wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa, ameitaka serikali kuweka mfumo wa kuzitambua bunifu za wazawa na kuziendeleza.

Aidha, Prof. Mganilwa alisema kwa hatua walipofikia wabunifu wazawa wanatakiwa kuungwa mkono na serikali na kuwaendeleza ili bunifu zao ziwe na tija.

Prof. Mganilwa alibainisha hayo jijini hapa katika kilelele cha mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

"Ni kweli vijana wetu wameonyesha uwezo mkubwa katika kubuni vitu vya kisayansi, serikali inatakiwa iweke mfumo mzuri wakuwaendeleza ili wabunifu hao waweze kuchangia Uchumi wa nchi," alisema.

Kwa upande wa NIT, alisema wanafunzi wa chuo hicho walikwenda katika maonyesho hayo na ubunifu wa sensor, ambayo inafungwa kwenye mabasi ili kumwelekeza abiria wapi anakwenda.

"Hii sensor inafungwa katika mabasi kama ya mwendokasi ambayo kazi yake ni kuonysha basi linaenda wapi pindi linapoingia kituoni," alisema Prof. Mganilwa.

Aidha, alisema teknolojia nyingine waliyokwenda nayo katika mashindano hayo ni maski ambayo hutumika kuvuta hewa ya oxygen kwenye ndege wakati inapokuwa angani kuanzia futi 20.

"Unajua ndege ikipaa juu kama futi 20, hewa yao (oksijeni) huwa inapungua, hivyo maski hiyo husaidia kuvuta hewa ya oksijeni," alisema.

Mashindano ya MAKISATU yalifanyika sambamba na maonesho ya wabunifu yaliyoanza Mei 6 na kumalizika jana.

Akiyafunga maonesho hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliziagiza taasisi na mamlaka ambazo zinashiriki kuendeleza wabunifu wachanga zihakikishe zinawawezesha kubiasharisha ubunifu na uvumbuzi wao.

## HABARI KITAIFA

# ‘95% wanaougua shinikizo la damu sababu hazijulikani’

**Na Christina Mwakangale**

IMEELEZWA asilimia 95 ya wagonjwa walio na shinikizo la juu la damu, sababu za kuugua hazijulikani kisayansi, huku kati yao wakirithi kutoka familia zao.

Aidha, duniani kati ya wanawake wanne mmoja ana tatizo hilo, huku mwanaume mmoja huugua kati ya wanaume watano.

Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), iliyasema hayo jana katika taarifa yake iliyotolewa na kitengo cha uhusiano na mawasiliano, kuadhimisha siku ya shinikizo la juu duniani, inayofanyika leo.

Taarifa hiyo, ilisema ugonjwa huo hutokana na baadhi ya watu kurithi kutoka kwenye familia zao na wengine kuupata kutoka na matatizo ya figo au kisukari.

“Matatizo yanayohisishwa na ugonjwa wa shinikizo la juu la damu ni uzito kupindukia, matumizi ya chumvi nyingi, uvutaji sigara, kutofanya mazoezi na ujauzito,” ilisema taarifa hiyo;

“Ulaji wa vyakula vya mafuta na wanga zaidi, umri mkubwa, msongo wa mawazo.”

Pia, JKCI ilibainisha kutokana na ongezeko la watu wanaougua ugonjwa huo duniani na kufikia bilioni moja, wakiwamo Watanzania, kwenye maadhimisho ya mwaka huu wametoa huduma ya vipimo bure kwa wakazi wa Manispaa ya Ubungo.

“Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), watu bilioni moja wana tatizo hili ikiwamo Tanzania. Hatari ya ugonjwa huu ni hauna dalili maalumu, ila linapodumu muda mrefu madhara ni makubwa kiafya na huharibu viungo vya mwili,” ilisema taarifa hiyo.

Kadhalika, katika maadhimisho hayo wakazi wa manispaa hiyo wakiwamo watu wazima na watoto, walipatiwa vipimo mbalimbali ikiwamo uzito, urefu, shinikizo la juu na kupewa ushauri. Pia waliogundulika na matatzo ikiwamo moyo, walipatiwa rufani ya kufanya uchunguzi zaidi ikiwamo matibabu katika taasisi hiyo na kwamba kaulimbiu mwaka huu ni ‘Pima shinikizo la damu, ishi maisha marefu’.

Aidha, taarifa hiyo ilisema madhara yatokanayo na ugonjwa huo ni kupunguza nguvu za kiume, kukosa hamu ya tendo la ndoa kwa wanawake, shambulio la moyo ama kushindwa kufanya kazi, kutanuka na kupata kiharusi.

“Madhara ya ugonjwa huu yanaweza kuepukwa kwa kufanya mazoezi, kupika afya kila mara, mlo wenye lishe na kufuata ushauri wa kitaalamu,” ilisema taarifa hiyo.

# TUSODARCO yapata rais mpya

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI ya Wanafunzi kwenye Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (TUSODARCo), sasa itaongozwa na Wilfred John baada ya kupata kura nyingi za urais dhidi ya wapinzani wake wawili ambao ni Lucian Lucelo na David Gasana.

Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi wa Chuo cha TUDARCO, Samuel Mmari, alimtangaza Willfred ambaye makamu wake ni Clara Danford kuwa mshindi baada ya kupata kura 362 kati ya 781 ambapo kura halali zilikuwa 778 zilizoharibika zilikuwa 3. Katika uchaguzi huo uliofanyika Mei 13, mwaka huu chuoni hapo, Mmari alitangaza kuwa Lucian ambaye makamu wake alikuwa ni Glory Muze ambaye alipata kura 270 wakati David na makamu wake Jaquline Kavishe aliambulia kura 146.

Kwa upande wa wabunge Jimbo la Mwenge lilinyakuliwa na George Helahela dhidi ya mpinzani wake, Amos Alipo, Sharifu Ramadhani (Jimbo la Kawe), Jimbo la Mikocheni litaongozwa na Hussen Issa wakati Judith Sichilima alinyakua Jimbo la Sinza akiwa ndiye mbunge pekee wa kike.

Akizungumzia badhiya ya vipaumbele vyake katika serikali yake Wilfred alisema amekusudia kushirikiana na uongozi wa chuo katika kutatua tatizo la uchache wa vitabu, ambapo atahamasisha kuimarishwa kwa mfumo wa WIFI, ambao anaamini utawezesha wanafunzi kupata vitabu vingine kwa kupitia intaneti kwenye chumba cha kompyuta chuoni.

“Siyo vitabu vyote tunaweza kuvinunua, kwenye suala la afya tutajitahidi kuwasiliana na wasimamizi wa mgahawa ili kuhakikisha tunapata chakula bora, lakini kiuzwe kwa bei ambayo wanafunzi wote wanamudu kununua, pia tunakusudia kuanzisha talent day (siku ya vipaji) ambayo mwanafunzi mwenye ubunifu wowote atatambuliwa na kupewa tuzo.”


**BUGANDO MEDICAL CENTRE**
**Consultant and Teaching Hospital**

## ADVERTISEMENT FOR

### Invitation for Submission of Tender Opportunity For Goods and Non - Consultancy Services

**Date: 17th May, 2021**

1. The Bugando Medical Centre has set aside funds towards the cost for the provision of various Goods and Non-Consultancy service and it intends to apply part of the proceeds of this funds towards the payments under the contract for:

   i. Provision of the supply of General Stationary and Medical stationary Printing at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/01

   ii. Provision of the supply of Medical Consumable and medical Equipment at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/02

   iii. Provision of the supply of Dressing, Uniform Bedding &Linen at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/03

   iv. Provision of the supply of Furniture and Fittings at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/04

   v. Provision of the supply of Cleaning & Crockery materials at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/05

   vi. Provision of the supply of Drugs at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/06

   vii. Provision of the supply of Building materials, hardware electrical and machinery (Engineering Material) at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/07

   viii. Provision of supply of Office Equipment (Computer and Accessories) at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/8

   ix. Provision of supply of Laboratory Reagents, chemicals and Laboratory Equipment at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/09

   x. Provision of supply of Medical Oxygen Gases at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/11

   xi. Provision of supply of Orthopedic Materials at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/12

   xii. Provision of supply of Haemodialysis Reagents at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/13

   xiii. Provision of supply of Dental Materials at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/14

   xiv. Provision of supply of Radiology Materials at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/15

   xv. Provision of supply of Food & Refreshment at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/16

   xvi. Provision of supply of Opthalmology Materials at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/G/2021-2022/17

   xvii. Provision of Repairs and maintaince Services of Motor Vehicles at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/NC/2021-2022/03

   xviii. Provision of the Maintenances and Services of hospital Fridges & Air conditioners at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/NC/2021-2022/04

   xix. Provision of the Services and Maintenances of Elevators at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/NC/2021-2022/10

   xx. Provision of the Services and Maintenances of Oxygen Plants , Air Compressor and Oxygen Fitting at Bugando Medical Centre Tender no. AP/161/HQ/NC/2021-2022/11

2. Tendering will be conducted through the National competitive Tendering (NCT) procedures specified in the Public Procurement (Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 Section 151) and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

3. Interested applicants may obtain information and the pre-qualification documents at the *Secretary of* ***BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza from 7:30 am to 15:30 pm local time*** on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

4. A complete set of pre-qualification documents in English may be purchased by interested Applicants on the submission of a written application to the address given under paragraph 3 above and upon payment of a non-refundable fee of [**One Hundred thousand only, TSH 100,000/=**]. Payment should be by Cash deposit into ***BMC Health Service Fund account no. 01J1051393600 CRDB bank*** and bring original pay slip

5. All applications one original plus **Two copies**, properly filled in, and enclosed in plain envelopes properly written the name of the tender, address, time and the word **“DO NOT OPEN BEFORE”** mentioned time of the deadline and must be delivered to the address ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza*** at or before ***10:00 am local time on 31st May, 2021.*** Applications will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Applicants’ representatives who choose to attend in the opening at the **Oncology Conference Hall.**

6. Late applications, portion of applications, electronic applications, applications not received, applications not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Dr. Fabian A. Massaga**
**Ag. Director General**
**P.O Box 1370,**
**Mwanza, Tanzania**
**Telephone 2540610/5 or 2500513**
**Fax: 255-028-2500799**
**Email: info@bugandomedicalcentre.go.tz/ hospbugando@gmail.com**

# Kanda ya Ziwa kinara magonjwa ya kichocho

**Na Neema Emmanuel**, MWANZA

ASILIMIA 50 hadi 90 ya wagonjwa milioni 22 walioambukizwa magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo wanatoka mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele mkoani Mwanza, Dk. Mabai Leonard.

Dk. Leonard alisema ugonjwa wa kichocho na minyoo ya tumbo bado ni tatizo mkoani humo.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo Mkoa wa Mwanza umeandaa kampeni ya utoaji wa dawa za kingatiba kwa watoto wa umri wa kwenda shule hadi miaka 15 wa shule za msingi zote kwa gharama ya Sh. milioni 288.4.

Alisema halmashauri zote mkoani Mwanza zihakikishe watoto watakaopewa dawa kinga wapate chakula saa mbili kabla ya kumeza dawa hizo aina ya Albendazole kwa ajili ya minyoo ya tumbo na Prazequantel ya kichocho na wapewe kulingana na urefu wao. Dk. Leonard alisema ugonjwa wa kichocho na minyoo ya tumbo hauna dalili za haraka kabla ya kupata matibabu hivyo kampeni ya kutoa dawa ya kingatiba inalenga kudhibiti na kutibu magonjwa hayo kwenye jamii.

Aliongeza kuwa tatizo la ugongwa wa kichocho na minyoo ya tumbo mkoani Mwanza linasababishwa na jiografia yake ya kuwa na maji mengi, shughuli za kilimo (majaruba ya mpunga) pamoja na maji ya madimbwi.

Aidha, Prof. Humphrey Mazigo wa Chuo Kikuu Katoliki cha Sayansi na Tiba za Afya Bugando (CUHAS), alisema magonjwa 17 kikiwamo kichocho na minyoo katika ukanda wa tropiki yanaikumba jamii maskini vijijini zinazoishi chini ya dola 2 za Marekani na zisizo na uwezo wa kugharamia tiba na athari.

Prof. Mazigo alisema Tanzania ni moja ya nchi zilizoathiriwa na ugonjwa wa kichocho hasa bonde la Ziwa Victoria hususani kwa wakulima, wavuvi na watoto na kwamba watu bilioni 2 duniani wameathirika na minyoo ya tumbo.

Alifafanua kuwa katika idadi hiyo watu milioni 300 wameathirika sana huku watu 155,000 kila mwaka duniani hufariki kutokana na magonjwa hayo.

Naye Kaimu Mratibu wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa hayo, Oscar Kaitaba, alisema yanaathiri maendeleo na makuzi ya watoto, kupunguza uwezo wa utendaji wa hivyo kusababisha umaskini kwenye jamii.

Alisema licha ya changamoto mbalimbali yapo mafanikio katika utoaji wa dawa za kingatiba kwenye halmashauri 184 nchini na kwamba kwa sasa maambukizi yamepungua kwenye halmashauri 71.

# Wazee wahakikishiwa matibabu bure ya CHF

**Na Marco Maduhu**, KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imewahakikishia wazee katika manispaa hiyo kuwa itaendelea kuwakatia bima ya afya ya CHF, ili waweze kupata matibabu bure katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za serikali.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Robert Kwela, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha kutathmini mradi wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wazee pamoja na upatikanaji wa matibabu bure.

Mradi huo unatekelezwa na Shirika la Tawlae linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga.

Alisema serikali wanathamini mchango wa wazee hapa nchini na ndiyo maana kila mwaka wa fedha, lazima waingize bajeti ya kukatia wazee bima hiyo ya afya CHF ili wapate matibabu bure bila ya usumbufu.

"Nalipongeza Shirika la Tawlae kwa kupigania haki za wazee na sisi kama serikali licha ya mradi wenu kuelekea mwisho lakini tutayaenzi yale mazuri ambayo mmetupatia ili kuhakikisha wazee hawa wanapata haki zote ikiwamo matibabu bure kwa kuwapatia bima za CHF," alisema Kwela.

Naye mratibu wa masuala ya wazee wa manispaa hiyo, Jonathani Shayo, alisema tangu mwaka 2018 hadi mwaka huu wameshatumia Sh. milioni 27.7 kwa ajili ya kukatia wazee bima hiyo ya afya CHF pamoja na kuimarisha huduma zao za matibabu.

Kwa upande wake, Katibu wa Baraza la Wazee Manispaa ya Kahama, Anderson Lyimo, alisema idadi yao inafikia 6,692, na kuipongeza serikali kwa kuwajali na kubainisha kuwaomba wadau wengine wajitokeze kuwakatia bima ya afya.

Katika hatua nyingine, alipongeza hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan, alipokuwa akizungumza na wazee kuwa imeonyesha matumaini kwao ikiwamo kupatiwa pensheni za uzeeni pamoja na kutungiwa sheria ya wazee.

Naye Ofisa Miradi kutoka Tawlae, Winie Hinaya, alisema walianza mpango wa kupambana na kutokomeza matukio ya ukatili kwa wazee mwaka jana.

## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED
## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

1st Housing

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2020 | Mwaka uliopita 31st Dec. 2019 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2 | 1,507 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 2,542,147 | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 8,921,407 | 14,892,541 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 6,254,136 | 2,040,750 |
| 12 | Mali Nyingine | 585,857 | 565,412 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 247,025 | 745,176 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **20,172,574** | **19,867,386** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 413,087 | 413,087 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 723,747 | 784,678 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 41,070 | 41,071 |
| 27 | Dhima Nyingine | - | 156,788 |
| 28 | Madeni | 1,010,479 | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **2,188,383** | **1,395,624** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **17,984,191** | **18,471,762** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,424,069) | (2,311,866) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (487,571) | (1,112,203) |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **17,984,191** | **18,471,762** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 135,854 | - |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 55,828 | 86,131 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 89.15% | 92.98% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.16% | - |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1525.46% | 497.12% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 31.00% | 10.27% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82.06% | 86.59% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0.00% | 15.10% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1.54% | -5.62% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| S/No | Maelezo | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2020 | Mwaka Uliopita 31st Dec. 2019 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,611,080 | 908,437 |
| 2 | Gharama za Riba | (35,911) | (60,415) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,575,169** | **848,022** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 47,524 | 18,539 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **24,001** | **63,497** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (2,622) | (3,719) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 7,650 | 7,850 |
| | 6.3 Gawio | 10,333 | 11,807 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 8,640 | 47,559 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(2,125,095)** | **(2,036,474)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (947,092) | (861,881) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,178,003) | (1,174,593) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(478,401)** | **(1,106,416)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (9,170) | (5,787) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(487,571)** | **(1,112,203)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | 95,831 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **(487,571)** | **(1,016,372)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 12 | 11 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (2.24) | (5.10) |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 |
| | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.44% | -4.97% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -2.67% | -5.35% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 129.97% | 209.53% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 9.33% | 8.86% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa (2020)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,424,069)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,471,762** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (487,571) | - | - | - | **(487,571)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,911,640)** | **-** | **-** | **95,831** | **17,984,191** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka uliopita (2019)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(2,321,223)** | **-** | **9,357** | **-** | **19,488,134** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (1,112,203) | - | - | - | **(1,112,203)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 9,357 | - | (9,357) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 95,831 | **95,831** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,424,069)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,471,762** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2020

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| S/No | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2020 | Mwaka Uliopita 31st Dec. 2019 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(478,401)** | **(1,106,416)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 517,159 | 549,318 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (4,213,845) | (1,105,208) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | - | 54,203 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (60,932) | (100,774) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (73,121) | (60,771) |
| | - Kodi iliyolipwa | (8,137) | (4,606) |
| | - Mengineyo | 20,157 | (334,206) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(4,297,120)** | **(2,108,460)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | 10,627 | 10,627 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (11,828) | (68,140) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | (485,098) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (2,720,274) | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,028) | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(2,723,503)** | **(542,611)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (Mkopo kutoka TMRC) | 1,000,000 | (142,239) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,000,000** | **(142,239)** |
| | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **(6,020,623)** | **(2,793,310)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 14,894,048 | 17,668,720 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 47,983 | 18,638 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **8,921,408** | **14,894,048** |




Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| Jina na Cheo : | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | 13.05.2021 |
| Amulike Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | 13.05.2021 |
| Ally Kimbulaga **(Kaimu Meneja - Mkaguzi wa Ndani)** | (Imesainiwa) | 13.05.2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| Jina: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sanjay Suchak Mwenyekiti | (Imesainiwa) | 13.05.2021 |
| Charles Itembe **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | 13.05.2021 |

Nipashe **Spotika**



WANAMICHEZO 10 DUNIANI WANAOLIPWA ZAIDI 2021 UK. 12-13



# MAKOCHA WANAOPASWA KUTIMULIWA MSIMU HUU

PIRLO

**ISIKUPITE**

MANCHESTER City ni timu ya kwanza katika historia ya Ligi Kuu England kutwaa ubingwa huo licha ya kuwa nafasi ya chini (ya nane) kwenye msimamo wa ligi hiyo Siku ya Krismasi, na ya kwanza katika timu za juu zinazowania ubingwa tangu Liverpool ilipofanya hivyo msimu wa 1981-82, ambapo ilikuwa nafasi ya 12 Siku ya Krismasi.



**LONDON,** England

TUMEONA idadi ya makocha wakubwa tayari wakiwa wamefukuzwa kazi mwaka huu na wengine wakitarajiwa mwishoni mwa msimu huu.

Tunaishi katika dunia ambayo mara zote imekuwa ikihitaji matokeo ya haraka na mara kwa mara wanasoka na makocha wamekuwa wakishutumiwa pale matokeo yanapokuwa tofauti na matarajio. Kwa mfano, Jose Mourinho anathibitisha hilo, hakufiti pale Tottenham Hotspur na wakaamua kumtimua. Na mfano kama huo unakwenda kwa Javi Gracia, ambaye amefukuzwa hivi karibuni na Valencia.

Kuna wakati baadhi ya klabu zinaamua kubakia na kocha hata kama kwa kipindi hicho matokeo si mazuri. Wakati mwingine makocha wanafukuzwa wanapoonekena kutofiti katika mahitaji ya klabu hata kama kuna matokeo mazuri. Maurizio Sarri ni mfano mzuri wakati alipofukuzwa Juventus.

Hapa tunawatazama makocha wanne ambao wanapaswa kufukuzwa mwishoni mwa msimu huu, wafahamu sasa...

**#4. WAYNE ROONEY - DERBY COUNTY**

Wayne Rooney aliteuliwa kuwa kocha wa Derby County Novemba mwaka jana baada ya kufukuzwa kwa Philip Cocu.

Novemba mwaka jana ilitangazwa kwamba, makubaliano yamefikiwa ili kuiuza klabu hiyo, lakini mpango huo ukasitishwa Machi mwaka huu.

Derby County iliepuka kushuka daraja baada ya kutoka sare ya mabao 3-3 na Sheffield Wednesday katika siku ya mwisho ya msimu uliopita. Derby County ilishinda mchezo mmoja tu kati ya 13 na sare ya siku ya mwisho ikawaokoa.

Derby County wanatakiwa kutafuta kocha mpya kama wanataka kurudi kwenye Ligi Kuu na watahitaji yule mwenye uzoefu wa kutosha. Rooney bado anaonekana hana uzoefu wa kuweza kuipandisha timu hiyo.

**#3. STEVE BRUCE - NEWCASTLE UNITED**

Mashabiki wa Newcastle United wameungana wanataka kocha wao afukuzwe, kwani hali yake kwenye Ligi Kuu ni mbaya.

Kelele za kutaka kufukuzwa kwa Bruce zimepazwa kwa muda mrefu na inashangaza kuona hadi sasa bado anadunda. Ripoti kadhaa zimedai kwamba, wamiliki wa klabu hiyo wamekuwa wakimwamini zaidi Bruce, lakini ukweli ni kwamba mashabiki wa timu hiyo wamemchoka.

Inaonyesha wazi kabisa kwamba, Bruce si mtu anayeweza kuiongoza Newcastle United kurudi kwenye ubora wake wa zamani.

**#2. MIKEL ARTETA - ARSENAL**

Mikel Arteta aliteuliwa kuwa kocha wa Arsenal na mashabiki walionekana kufurahia ujio wake. Arteta pia aliiongoza klabu hiyo kwenye ushindi wa Kombe la FA msimu wake wa kwanza, lakini tangu hapo ameonyesha kuwa si mtu sahihi kwa klabu hiyo.

Arsenal ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu na wanaonekana wanaweza kushindwa kufuzu kucheza mashindano ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 1995-96. Walitupwa nje kwenye nusu fainali ya Ligi ya Europa na Villarreal na mashabiki sasa wanataka Arteta afukuzwe.

Mashabiki mara kwa mara wamekuwa hawaridhishiwa na chaguo la timu la Arteta na hasa kwa sababu klabu ilimuunga mkono kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Huku usajili wa pauni milioni 45 wa Thomas Partey ukionekana kutolipa, Willian ameshindwa kabisa kuonyesha ubora wake. Arsenal inapambana kumaliza ligi katika tano bora ili iweze kupata nafasi ya kufuzu kucheza Ulaya.

**#1. ANDREA PIRLO - JUVENTUS**

Juventus ni klabu ambayo ilimfukuza Maurizio Sarri licha ya kushinda taji la Ligi Kuu Italia kwenye msimu wake wa kwanza, imeonyesha kumvumilia sana Andrea Pirlo hadi sasa.

Juve ya Pirlo haikuwapo kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, na sasa wapo nafasi ya tano kwenye msimamo. Hivi karibuni walikumbana na kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa AC Milan na sasa wanaanza kupoteza imani na kocha wao huyo.

Hata hivyo, Pirlo mwenyewe ameshaibuka na kusema kwamba, hawezi kujiuzulu katika nafasi hiyo kwa sasa.

Akizungumza na Sky Sports baada ya kichapo hicho cha 3-0, Pirlo alisema: "Kujiuzulu? Hapana, sitafanya hivyo. Nilichukua jukumu hili kwa shauku kubwa nikijua kuna kipindi nitapitia magumu, hivyo nitaendelea kufanya kazi yangu."

Juventus ilishinda mara tisa mfululizo taji la Serie A kabla ya Pirlo kuchukua mikoba na sasa wapo kwenye hatari ya kushindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.



# WANAMICHEZO 10 DUNIANI WANAOLIPWA ZAIDI 2021

**LONDON,** Egland

MICHEZO imeendelea kuwa moja ya sehemu bora kabisa ya burudani, na wanamichezo wakubwa wamekuwa wakifurahia miaka yao mizuri kwenye michezo mbalimbali.

**Kumekuwa na tatizo la kifedha kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, lakini wanamichezo wameendelea kuingiza kiasi kikubwa cha fedha. Ukiacha mishahara yao, wanamichezo kadhaa wamekuwa wakiendesha biashara zao ambazo zimekuwa zikifanya vizuri.**

Pamoja na hilo, makampuni makubwa yamekuwa yakitoa udhamini kwa wachezaji kwa kutangaza bidhaa zao na wamekuwa wakiwalipa fedha ndefu.

Mpira wa kikapu na mpira wa miguu, imebakia kuwa michezo maarufu zaidi duniani, huku soka la Marekani pia likitoa uwakilishi.

Makala haya yanawaangalia wanamichezo 10 ambao wanalipwa zaidi duniani kwa mwaka huu, twende sasa...

### #10. KEVIN DURANT | DOLA MIL. 75

Kevin Durant, mara kwa mara amekuwa akiitwa "KD", ni mmoja wa wachezaji wa mpira wa kikapu maarufu zaidi duniani.

Durant amefurahia maisha yake kwenye mchezo huo, akiwa ameshinda mataji mawili ya NBA, tuzo ya mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi wa NBA, na medali mbili za Olimpiki. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, kwa sasa anaichezea timu ya Brooklyn Nets, awali alikuwa akiichezea Golden State Warriors.

Ni wakati akiwa na Golden State Warriors ndipo Durant alishinda taji la NBA mara mbili mfululizo, mwaka 2017 na 2018. Alichelewa kuanza kuichezea Brooklyn Nets kutokana na kuwa majeruhi, lakini uwezo wa Durant umeendelea kumfanya kuwa mchezaji bora.

### #9. TOM BRADY | DOLA MIL. 76

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora wa muda wote kwenye soka la Marekani.

Brady alitumia miaka yake 20 ya kwanza akiichezea New England Patriots, ambako aliisaidia timu hiyo kushinda mataji sita makubwa ya Super Bowl na 17 ya kanda. Muda wake na New England Patriots ulimalizika mwaka 2019, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 43 kwa sasa, akajiunga na Tampa Bay Buccaneers.

Akiwa na Tampa Bay Buccaneers, Brady tayari ameshinda taji kubwa la Super Bowl mwaka huu na kutajwa kuwa mchezaji mwenye thamani kubwa kwenye Super Bowl.

### #8. LEWIS HAMILTON | DOLA MIL. 82

Pengine ndiye dereva wa mbio za magari maarufu zaidi kwa sasa, Lewis Hamilton amekuwa na wakati mzuri kwenye mashindano ya Formula One.

Muingereza huyu kwa sasa kwenye mashindano ya Formula One yupo na timu ya Mercedes, akiwa ameanzia kule McLaren. Hamilton ameshinda mataji saba ya dunia, huku akiweka rekodi kadhaa binafsi. Hamilton mwenye umri wa miaka 36, anachukuliwa kama mmoja wa madereva wanaowavutia vijana wengi duniani.

### #7. ROGER FEDERER | DOLA MIL. 90

Pengine ndiye mchezaji bora zaidi wa wakati wote wa tenisi duniani, Roger Federer ndiye anayeongoza kwa kulipwa zaidi katika mchezo huo.

Federer raia wa Uswisi, ameshinda mataji 20 ya Grand Slam, na amekuwa na upinzani mkubwa na Rafael Nadal kabla ya Novak Djokovic.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 39, kwa sasa anashika nafasi ya nane katika viwango vya ubora wa wachezaji wa tenisi duniani.

### #6. NEYMAR | DOLA MIL. 95

Nyota huyu wa Paris Saint-Germain, Neymar haitaji maneno mengi kumtambulisha kama mmoja wa mastraika bora wa soka duniani.

Neymar alianza kucheza soka la Ulaya akiwa na Barcelona, akitengeneza upatina mzuri na Lionel Messi na Luis Suarez. Watatu hao kwa pamoja walikuwa na mchango mkubwa wakati Barcelona ikishinda mataji matatu chini ya utawala wa Luis Enrique.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, aliamua kujiunga na Paris Saint-Germain kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya Euro milioni 222 mwaka 2017, na Neymar amekuwa nguzo kubwa tangu kutua hapo Paris. Katika mechi 114 alizoichezea Brazil kwenye mashindano yote, amefunga mabao 86. Neymar hivi karibuni alisaini mkataba mpya na miamba hao wa Ligue 1.

### #5. LEBRON JAMES | DOLA MIL. 96.5

LeBron James mara kwa mara amekuwa akilinganishwa na Michael Jordan, kama mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea kwenye mchezo wa mpira wa kikapu.

Akiwa bado yupo imara katika umri wake wa miaka 36, James alianza kuichezea Cleveland Cavaliers, baadaye akajiunga na Miami Heat katika usajili wa utata mwaka 2010. Akiwa na Heat, James alishinda mataji mawili ya NBA, kabla ya kurudi Cleveland Cavaliers mwaka 2014 na kuiongoza kushinda taji mwaka 2016.

James kwa sasa anaichezea Los Angeles Lakers na ameshinda taji la NBA mwaka 2020. Raia huyo wa Marekani ameshinda mataji manne ya NBA na kuwa MVP na kutwaa medali mbili za Olimpiki.

### #4. DAK PRESCOTT | DOLA MIL. 105.5

Ni nyota wa timu ya soka la Marekani ya Dallas Cowboys, Dak Prescott, hivi karibuni alisaini kuongeza mkataba mpya.

Prescott alichaguliwa kama mchezaji bora wa wakati wote wa Dallas Cowboys mwaka 2016 na ameshinda nao taji la Ligi Kuu ya NFL kila mwaka hadi sasa. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 pia ana rekodi zake kadhaa.

### #3. CRISTIANO RONALDO | DOLA MIL. 120

Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora zaidi duniani kwa sasa akiwa anakipiga kule Juventus.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alitengeneza jina lake akiwa na Manchester United, akishinda mataji matatu ya Ligi Kuu England na Kombe la Corobao. Alihamia Real Madrid mwaka 2009 kwa ada iliyoweka rekodi kipindi hicho ya Euro milioni 94 na akawa mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, ambaye ameshinda mataji matano ya Ballon d'Or, matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na moja la Ligi ya Europa, amekuwa akihusishwa na mapango wa kurudi Manchester United.

### #2. LIONEL MESSI | DOLA MIL. 130

Pengine ndiye mchezaji soka bora zaidi wa muda wote, Lionel Messi amefurahia kipindi chake akiwa na Barcelona.

Messi mwenye umri wa miaka 33, amecheza mechi 777 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo, akifunga mabao 671.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, mkataba wake na Barcelona unamalizika kipindi hiki cha majira ya joto na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Manchester City na Paris Saint-Germain. Hata hivyo, uvumi wa hivi karibuni umedai kwamba, anaweza kusaini mkataba mpya wa kubakia hapo Camp Nou.

### #1. CONOR MCGREGOR | DOLA MIL. 180

Mwanamasumbwi aliyejichanganya kwenye 'martial arts' Conor McGregor, ndiye mwanamichezo anayelipwa zaidi duniani.

Imekuwa ikiripotiwa kwamba, kiasi kikubwa cha fedha nyingine anakiingiza kutokana na biashara zake nyingine. Nyota huyu kutoka Ireland amekuwa ni mtata mno katika maisha yake ya kimichezo.

Katika umri wake wa miaka 32, mara zote mapambano yake yamekuwa yakiwavutia wengi na kufanya biashara kubwa. McGregor alianza masumbwi kwa kucheza na Floyd Mayweather Jr. na alipigwa.

MCGREGOR

## Nukuu

"Tuko katikati ya mchakato. Tuna nafasi nzuri (ya kujijenga upya), ninafurahi sana kwa sababu najua nini tutakachoweza kufanya kwa saizi na rasilimali tutakayokuwa nayo. Nadhani wamiliki watahusika sana na kuunga mkono, " **Kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta**



"Huu umekuwa msimu wa taji la Ligi Kuu kama hakuna mwingine. Hii ilikuwa ngumu zaidi. Tutaukumbuka msimu huu wakati wote kwa namna tulivyoshinda. Ninajivunia sana kuwa kocha hapa na wa kundi hili la wachezaji," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola baada ya kutwaa ubingwa.**



"Kujiuzulu? Hapana, sitaachia ngazi. Nilichukua jukumu hili kwa shauku kubwa wakati wa shida kadhaa. Mimi nisiyefaa klabuni, kwa hiyo nitaendelea kufanya kazi yangu maadamu naruhusiwa," **Kocha wa Juventus, Andrea Pirlo.**






Winga wa Simba, Luis Miquissone akiambaa na mpira dhidi ya beki wa Kaizer Chiefs kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa FNB, Afrika Kusini juzi. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA NA REKODI ZA KUPINDUA MEZA CAF

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha mabao 4-0 ilichokipata Simba dhidi ya Kaizer Chiefs kwenye Uwanja wa FNB nchini Afrika Kusini kimeiweka timu hiyo kwenye wakati mgumu wa kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Yalikuwa ni mabao mawili ya Mserbia Samir Nurkovic, Mcolombia Leonardo Castro, na Msauzi Erick Mathoho, yaliyotosha kuwaangamiza 'Wekundu wa Msimbazi' hao, hivyo sasa kuhitaji kushinda 5-0 kwenye mechi ya marudiano, Jumamosi ili kusonga mbele kwenye hatua hiyo.**

Ni mechi ambayo imeacha maswali mengi kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo, wakiwa hawaamini kilichotokea hasa ikizingatiwa kikosi cha msimu huu kilivyokuwa bora kwenye michuano hiyo na Ligi Kuu, lakini wapinzani wao Kaizer Chiefs wakiwa hawafanyi vema kwenye Ligi Kuu Aftika Kusini.

Simba ina rekodi kadhaa ya kupindua mechi kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa. Lakini kwenye mechi hii inaweza kushinda idadi ya mabao 5-0? Makala haya yanakuletea mechi ambazo Simba imeshawahi kusonga mbele kwenye mazingira ambayo hayakutarajiwa, twende sasa...

### #1. KUICHAPA MUFULIRA WANDERERS 5-0 NYUMBANI KWAO

Ni rekodi ambayo hadi leo ipo kwenye Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na kila mwaka huweka kumbukumbu hiyo kwenye moja ya mambo ya kukumbukwa katika soka la Afrika.

Ni pale Simba ilipoifunga Mufulira Wanderers ya Zambia mabao 5-0 ikiwa ugenini nchini Zambia, ikiwa imetoka kufungwa mabao 4-0 nchini Tanzania.

Hakuna aliyetarajiwa. Simba ilichapwa mabao 4-0 Dar es Salaam na kila mmoja alijua kuwa inakwenda kukamilisha ratiba tu kwenye mechi ya marudiano nchini Zambia.

Hata watangazaji wa Redio Tanzania Dar es Salaam wakati huo walishindwa kuungana na wachezaji kwenda kwenye mechi hiyo.

Baadhi ya viongozi wa Simba walikata tamaa na hata maaandalizi yalikuwa ya kuungaunga.

Wachezaji wa Simba walisafiri kwa treni ya TAZARA hadi Zambia kwenda kukamilisha ratiba. Ilikuwa taarifa ya habari ya saa 2:00 usiku wakati mtangazaji alipotangaza matokeo ya mechi hiyo.

Simba ilishinda mechi hiyo mbele ya Rais wa nchi hiyo, Kenneth Kaunda aliyekuwa mgeni rasmi na ikasonga mbele kwa jumla ya mabao 5-4. Hakuna aliyeamini. Kilichofuata ni shamrashamra nchi nzima, huku wakiuliza ilikuwaje? Lakini yalikuwa ni mabao ya Thuwein Ally aliyefunga mabao matatu na Geogre Kulagwa mawili.

### #2. KUIVUA ZAMALEK UBINGWA WA AFRIKA

Mechi nyingine ambayo Simba ilipindua meza, vile vile ikiwa ugenini ilikuwa ni Juni Mosi, 2003 nchini Misri ilipoivua Ubingwa wa Afrika, Zamalek na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa.

Nayo ilikuwa kama mzaha tu. Ilishinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam sasa Uhuru, lililofungwa na Emmanuel Gabriel.

Ushindi huo mwembamba uliwatia mashaka mashabiki wengi hasa ikizingatia si tu ilikwenda kucheza ugenini na timu ya Afrika Kaskazini maarufu kama timu ya 'Uarabuni' ambao walikuwa hawafungiki kwao, lakini pia Mabingwa Watetezi wa Afrika.

Simba ilipindua matokeo kwa kuzuia kufungwa mabao mengi. Ikafungwa 1-0 tu. Timu zikaenda kwenye matuta.

Simba ilisonga mbele kwa penalti 3-2, Juma Kaseja akiokoa mbili, marehemu Christopha Alex akienda kupiga penalti ya mwisho na ya ushindi.

### #3. ILIVYOINYANG'ANYA TONGE NKANA FC

Ilikuwa ni Desemba 23, 2018 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Simba ilipopindua meza kwa Nkana FC ambao kabla ya dakika mbili mpira kwisha walikuwa na uhakika kwenda kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mashabiki wa Simba walikuwa kimya, lakini bao la dakika ya 88 la Clatous Chama, lilitosha kuipeleka Simba hatua ya makundi kwa ushindi wa mabao 3-1.

Kabla ya bao hilo, Simba ilikuwa inaongoza 2-1, ushindi ambao bado haukuihakikisha kusonga mbele.

Ni kwa sababu ilikuwa imefungwa mabao 2-1 nchini Zambia Desemba 15, mwaka huo huo na ilihitaji ushindi zaidi ili kupindua matokeo.

Jonas Mkude na Meddie Kagere walitangulia kuipatia Simba mabao mawili ya kwanza, John Bocco akifunga la kufutia machozi ugenini.

### #4. ILIPOISHANGAZA VITA CLUB DAR

Mwaka 2019, Vita Club ilihitaji sare tu ili kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Ikiwa na matumaini makubwa baada ya kushinda mabao 5-0 nchini DR Congo, ilitegemea kupata angalau sare ili kuweza kutinga hatua hiyo.

Simba ililazimika kushinda ili kuweza kutinga hatua ya robo fainali. Na kweli Vita Club ilipata bao la kuongoza na kuifanya Simba kuwa kwenye mlima mrefu.

Mohamed Hussein alirahisisha kazi na kufunga bao la kusawazisha. Ilikuwa imesalia dakika moja tu, Vita Club kuweza kutinga hatua ya robo fainali, lakini Chama alifunga bao dakika za mwisho na kupindua meza, Simba ikienda kwenye hatua hiyo kibabe.

Lakini je, itaweza tena kufanya hivyo kwa kupindua meza dhidi ya Kaizer Chiefs kwa ushindi wa mabao 5-0, ili kutinga nusu fainali? Ni suala la kusubiri na kuona.

## JE, WAJUA?



MIKEL Arteta (miaka 37 na siku 49) ni kocha mdogo zaidi katika historia ya Ligi Kuu England kumaliza msimu wa ligi hiyo kwa kuifunga Chelsea nyumbani na ugenini.



HABARI DODOMA

# Pinda ataka miti iliyopandwa kutunzwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, amewataka wakazi wa Dodoma kuitunza miti iliyopandwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa katika kampeni ya upandaji miti 10,000, Kata ya Zuzu iliyodhaminiwa na Benki ya Exim kwa kushirikiana na Taasisi ya Habari Development.

Alisema miti iliyopandwa kwenye eneo hilo itasaidia kubadilisha hali ya hewa endapo jamii itahamasishwa kuendelea kupanda na kuitunza.

"Kumekuwa na hewa chafu inayosababishwa na uchomaji taka mbalimbali katika viwanda, lakini miti ikiwapo husaidia kupunguza hewa chafu na kuleta safi ndio maana tunasisitiza miti ipandwe na kutunzwa ili kuikijanisha Dodoma," alisema Pinda.

Awali, akimkaribisha Pinda, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, alisema serikali itahakikisha Shule ya Sekondari ya Zinje inapata kisima cha maji kwa ajili umwagilia miti hiyo.

Aliutaka uongozi wa shule hiyo kufika ofisini kwake kwa ajili ya kukabidhiwa mhandisi ambaye atawapa michoro na kupima eneo lenye maji ili uchimbaji wa kisima hicho uanze.

Kwa upande wake, Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema benki hiyo itashirikiana na serikali kuhakikisha shule hiyo inapata visima vya maji ili kutunza miti hiyo.

Alisema katika kampeni hiyo wamejipanga kushiriki kikamilifu kuhakikisha wanafanikisha upandaji miti Dodoma.

Naye Katibu wa Habari Development, Bernard James, alisema taasisi hiyo imelenga kuhakikisha kampeni hiyo inafanikiwa na kuchangia kubadilisha hali ya hewa na kuleta rutuba katika ardhi.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akipanda mti jana Shule ya Sekondari Zinje iliyopo Kata ya Zuzu mkoani Dodoma, katika kampeni za kuikijanisha Dodoma, kushoto ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wajasiriamali wazindua umoja kutafuta soko

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIKUNDI vya wajasiriamali Mkoa wa Dodoma vimezindua umoja wao utakaosaidia kutafuta fursa za masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

Umoja huo unaojulikana kama 'Kijiji kipya' pia utawanufaisha na programu za mafunzo zitakazotolewa na serikali ya Korea Kusini.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Katibu wa umoja huo mkoani humo, Christopher Dioniz, alisema kuwa kijiji kipya ni mtandao wa pamoja na taasisi ya mama ya Saemoul Undong ya nchini Korea Kusini.

"Kwa hapa nchini kijiji kipya kinaundwa na vikundi jamii vya wajasiriamali vikiwamo vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambavyo vinapata mikopo ya asilimia 10, inayotengwa na serikali kupitia halmashauri zake," alisema Dioniz.

Alisema umoja huo unalenga kukusanya watu na kuwaunganisha ili kuwa na nguvu ya pamoja na kujiletea maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na mazingira.

Katibu huyo alisema umoja huo utajenga ari ya wananchi kuwa na moyo wa kujiamini, kujituma, kujitolea na kushirikiana kwa lengo la kujiletea maendeleo na maisha bora na kushirikiana na serikali na asasi zingine za kiraia kitaifa na kimataifa.

"Pia kijiji kipya kitafanyika benki ya habari kwa wanakijiji (vikundi) ili kupata taarifa za masoko, kubadilishana uzoefu kati ya kikundi na kikundi na kuboresha utendaji wa vikundi kutokana na mafunzo mbalimbali yatokayotolewa ndani na nje ya nchi," alisema Dioniz.

Alisema mpaka sasa umoja huo umefungua matawi yake katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Ruvuma, Morogoro na Dodoma na lengo ni kufika katika maeneo yote nchini.

Naye Mratibu wa Kijiji kipya nchini, Henry Mbwambo, alisema programu za mafunzo ambazo zitatolewa na Serikali ya Korea Kusini itahusisha wanavikundi pamoja na maofisa wa serikali.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo katika sekta za uzalishaji mali ili kukuza mitaji yao kama ambavyo vikundi vilivyopo nchini Korea Kusini vilivyopiga hatua.

"Dhana ya kijiji kipya inatokana na neno la Kikorea la 'Saemoul Undong' ikimaanisha kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kufikia mafanikio na kuachana na utegemezi," alisema Mbwambo.

Akizindua umoja huo, Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, aliwataka kushirikiana ili kufikia malengo kwa kubadilishana uzoefu.

# Askofu ataka ushirikishaji wananchi kwenye miradi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Assemblies of God Tanzania, Dk. Daniel Awet, ameiomba serikali kushirikisha jamii inapotekeleza miradi ya maendeleo ili kuondoa migogoro itakayojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi.

Dk. Awet alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na maaskofu, wachungaji na watumishi wa idara mbalimbali za kanisa hilo kwenye uzinduzi wa mpango mkakati wao wa miaka 10 uliofanyika kanisa la PAG jijini hapa.

Alisema pia Watanzania watoe ushirikiano kwa serikali inapopeleka miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Pia Watanzania tuendelee kuiombea serikali yetu iendelee kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo ile ya kiserikali na madhehebu ya dini," alisema.

Akizungumzia mkakati ya kanisa hilo, alisema kuwa kwa mwaka huu wameandaa mpango mkakati utakaosaidia katika kuongeza kasi ya upelekaji wa injili na usimamizi imara wa miradi waliyonayo.

Alisema kuwa taasisi isipokuwa na mpango mkakati haiwezi kuendelea, kanisa hilo limeandaa mkakati wake kwa mara ya kwanza wa miaka 10 ambao utakuwa na malengo 13.

Aliwataka viongozi na waumini wa kanisa hilo, kufanya kazi kwa mujibu wa mpango mkakati unavyoelekeza ili kufikia malengo yao kimaendeleo.

Naye Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo wa kanisa hilo, Mchungaji James Kesanta, alisema kuwa mpango mkakati ulianza kuandaliwa tangu mwezi Februari 2020, lakini huchukua muda mrefu kuukamilisha kutokana na tatizo la ugonjwa wa corona ulioikumba Tanzania na ulimwengu.

Alisema kuwa mpango mkakati huo uliundwa na timu ya watu 10 kutoka sehemu mbalimbali wakiwakilisha idara na taaluma mbalimbali wakiwamo, ofisa elimu wilaya, maaskofu, mwakilishi wa kanisa hilo Canada, vijana, idara ya maendeleo ya jamii na kiongozi wa umisheni na uinjilisti.

"Tangu mwaka 1950 kanisa halijawahi kuwa na mpango mkakati hivyo mpango mkakati ndio unaotoa dira kuwa kanisa limetoka wapi, lipo wapi na linaelekea wapi, nampongeza Askofu Awet kwa kubuni mpango mkakati huu," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii wa kanisa hilo, Getrude Majaliwa, alisema kuwa mpango mkakati huo utakuwa na tija kubwa kwa maendeleo ya kanisa kwa kuwa umejikita kuinua uchumi wa waumini wa kanisa hilo.

Naibu Katibu Mkuu wa kanisa hilo, Mchungaji Charles Kanyika, alisema kuwa kwa sasa kuna washirika 57,000 na katika mpango huo matarajio ni kufikia washirika 580,000.



## HABARI MBEYA



Askari mkoani Mbeya, akiwapanga watu wenye mahitaji maalumu kwenye lango kuu la kuingilia Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, waliojitokeza kuomba misaada kwenye ibada ya sikukuu ya Eid El Fitr huku aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila akitoka uwanjani hapo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wadau watoa ushauri udhibiti hewa ya ukaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa mazingira wamewashauri wananchi kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo yao ili kuepuka madhara yanayotokana na uchafuzi huo, ikiwamo kuchangia uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Ushauri huo ulitolewa juzi na wadau wa mazingira kutoka Shirika la Maendeleo na Utunzaji wa Mazingira Tanzania (SMT) walipokuwa wanatoa elimu ya mazingira kwenye shule za msingi na sekondari za Jiji la Mbeya.

Akizungumza wakati wa kutoa elimu hiyo kwenye Shule za Msingi Nzovwe na Shule ya Sekondari Nzondahaki kwenye Kata ya Nzovwe, Mkurugenzi wa Shirika la SMT, Paulo Masasi, alisema tatizo la uharibifu wa mazingira nchini limeendelea kuwa tatizo.

Alisema uharibifu wa mazingira umekuwa ukitokea kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwamo ukataji miti kwa ajili ya kuni, mkaa, shughuli za kilimo pamoja na shughuli za ujenzi.

Alisema kutokana na hali hiyo ndiyo maana waliamua kuanza kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii, wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ili kuimarisha utamaduni wa kutunza mazingira kwenye jamii.

"Tunatoa elimu ya upandaji miti na kuitunza ili kuyafanya mazingira kuwa rafiki kwa maisha ya binadamu, lakini tunatoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwenye jamii yetu, sasa tumeanzia kwa wanafunzi kwa sababu hili ni kundi kubwa na ni rahisi kueneza elimu hii," alisema Masasi.

Alisema mbali na kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi, pia wanatoa elimu kwa taasisi mbalimbali za umma na kwamba katika Mkoa wa Mbeya watatoa elimu hiyo kwenye halmashauri mbalimbali.

Mhamasishaji wa Utunzaji wa Mazingira wa Shirika hilo la SMT, Sani Kaloloma, alisema uzalishaji wa hewa ya ukaa duniani umekuwa ukiongezeka hali ambayo inasababisha uharibifu wa Tabaka la Ozoni na kuongezeka kwa joto duniani.

Alisema utunzaji wa mazingira ni miongoni mwa malengo ya maendeleo endelevu ya dunia, hivyo wao kama wadau ni lazima washirikiane na serikali kutoa elimu na hamasa kwa jamii.

Alisema mbali na kutoa elimu pia wanashiriki kupanda miti ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda, kivuli na ya kutunza vyanzo vya maji kwenye maeneo tofauti.

"Tunachokihitaji sio matunda tu bali ni pamoja na miti mingine kwa sababu moja kati ya faida za miti ni pamoja na kufyonza hewa ya ukaa ambayo imekuwa ikizalishwa viwandani na maeneo mengine," alisema Kaloloma.

Mwenyekiti wa Shirika hilo, Nestory Malembo, alisema wanafunzi ni rahisi zaidi kuwafundisha na wao wakafikisha elimu kwenye jamii wanazotokea kuliko kutoa elimu kwa watu wazima pekee.

Nao walimu wa mazingira kutoka katika shule ambazo zilifikiwa na elimu hiyo walisema elimu waliyopewa wanafunzi wao itasaidia kukatika utunzaji wa mazingira kwenye taasisi hizo.

Mwalimu wa Mazingira wa Shule ya Msingi, Nzovwe, Anna Mlatha, alisema wamekuwa wakitoa elimu hiyo kwa wanafunzi lakini kutokana na shirika hilo la SMT kuanza kushirikiana nao wana uhakika itafika kwa usahihi kwenye jamii.

# Sababu kampuni za ulinzi, wateja kuvunja mikataba hii

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

UCHELEWESHAJI wa leseni za umiliki wa silaha kwa kampuni binafsi za ulinzi nchini, umedaiwa kuwa chanzo cha kampuni hizo kuvunja mikataba na wateja wao, hivyo kuzifanya zikose fedha kwa ajili ya kuwalipa watumishi wao wakiwamo walinzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu wa Chama cha Sekta Binafsi ya Ulinzi Tanzania (TSIA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Hokololo, wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho uliofanyika jijini Mbeya.

Alisema baadhi ya wateja wa kampuni hizo huwa wanataka walinzi wenye silaha za kisasa hasa bunduki na hivyo ili wapate kazi kwa wateja wa aina hiyo huwa wanalazimika kununua silaha hizo, lakini wanashindwa kuzitumia kwa sababu ya ucheleweshaji wa vibali vya umiliki.

Alisema ili wapate kazi kwa wateja hao huwa wanalazimika kuonyesha risiti za kununulia silaha hizo, lakini vibali huwa vinachelewa mpaka zaidi ya miezi sita, hivyo wateja kuamua kuvunja mikataba na kutafuta wateja wengine.

"Mteja akishavunja mkataba, sisi tunaanza kukosa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa kampuni ikiwamo kuwalipa walinzi, sasa ukishindwa kuwalipa ndipo migogoro huwa inaanza na hata uharifu huwa unaongezeka, hivyo tunaomba tuangaliwe vizuri," alisema Hokololo.

Nao baadhi ya wamiliki wa kampuni hizo walisema tatizo lingine linalozikabili kampuni hizo ni taasisi za serikali wanazofanya nazo kazi kushindwa kuwalipa kwa wakati fedha zao.

Mmoja wa wamiliki wa Kampuni hizo, Vicent Kalindila, alisema wanafanya kazi na halmashauri na ofisi za wakuu wa mikoa lakini huwa haziwalipi, hivyo kuwa sehemu ya wasababisha migogoro kwenye kampuni.

Alisema mara nyingi halmashauri hizo zinapoingia mikataba na kampuni ya ulinzi huwa zinawaaminisha kuwa bajeti ya kuwalipa ipo, lakini muda ukifika huwa haziwalipi.

"Serikali huwa inatuona mara nyingi sisi kwamba ni wasumbufu, lakini kiuhalisia taasisi zake ndizo huwa zinasababisha baadhi ya usumbufu huo, kwa hiyo tunaomba sana tusaidiwe," alisema Kalindila.

Naye Vailet Kasamala alisema walinzi wanapocheleweshewa malipo yao huwa wanaingia tamaa ya kuanza kuchukua vitu vya wateja wa kampuni hizo ili wakajikimu na familia zao hali ambayo alisema huwa inazalisha migogoro mingine.

Alisema baadhi ya kampuni hizo zimekuwa zikiingia gharama kubwa ya kuwalipa wateja wao baada ya vitu kupotea kwenye malindo yao na kwamba mara nyingi vitu hivyo huwa vinachukuliwa na walinzi hasa wanapokuwa hawajalipwa mishahara.

Akijibu kero hizo, Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Max Mathayo, alikiri uwepo wa ucheleweshaji wa vibali vya umiliki wa silaha kwa kampuni hizo.

Alisema vibali hivyo huwa vinacheleweshwa kutokana na mchakato wake kuwa mrefu na huwa unatakiwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kujiridhisha.

# Mtuhumiwa wa ujambazi auawa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MTU asiyefahamika jina wala makazi yake ambaye anadhaniwa kuwa jambazi, ameuawa na wananchi, huku wenzake wakitimua mbio na kutokomea kusikojulikana katika Kitongoji cha Igundu kilichopo Kata ya Sangambi wilayani Chunya.

Inadaiwa tukio hilo liliitokea baada ya kundi la watuhumiwa wa ujambazi hao kutaka kuvamia soko la dhahabu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema katika tukio hilo majambazi hayo yalitelekeza silaha moja aina ya shortgun na risasi tatu.

Alisema jeshi hilo linaendelea kuwasaka majambazi wengine waliotimka mbio kwenye huku akiwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kufanikisha kukamatwa kwa majambazi hao.

"Natoa wito kwa jamii kuwafichua wahalifu kabla hawajatekeleza uhalifu wao, lakini wananchi waache kujichukulia sheria mkononi maana wanaharibu ushahidi," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na pombe haramu ya moshi kufuatia msako uliofanywa kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya.

Alisema katika tukio la kwanza jeshi hilo lilimkamata, Elizabeth Leonard (33) mkazi wa Mtaa wa Iwambala katika Jiji hilo akiwa na lita tano za gongo.

Alisema mthumiwa alikamatwa Mei 12, mwaka huu saa 5:30 asubuhi na kwamba mtuhumiwa ni mtengenezaji, mtumiaji na mfanyabiashara wa pombe hiyo.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine kuwa ni John Benard (44), mkazi wa Ipinda wilayani Kyela ambaye alikutwa na pombe hiyo ya moshi yenye ujazo wa lita 25.

Aliwataka wananchi kuacha kutumia pombe hiyo akidai kuwa ni hatari kwa afya zao, hivyo akasisitiza kuwa jeshi hilo litaendelea kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaofanya biashara hiyo.





# ‘TASAF kimbilio la kaya maskini’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Omar Mchengerwa, amesema lengo la Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ni kuwajengea uwezo wananchi wa kaya maskini.

Alisema kila mtu anafahamu kuwa Watanzania walio wengi ni maskini wa kipato na mfuko huo ndio kimbilio kwa wananchi hao wenye kuishi katika kaya hizo.

Alisema hayo wakati akikagua ukumbi wa kufanyia mtihani kwa wanafunzi wa kidato cha nne na pili, katika Shule ya Fujoni, Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Alisema jengo hilo lililojengwa na TASAF ni moja ya mafanikio ya maendeleo kwa wananchi wa kijiji cha Fujoni na wanafunzi wa shule hiyo kwa vile walikuwa wanafanya mitihani yao wakiwa wamekaa chini ya miti.

Alisema kwa sasa Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania imepanga kuipatia Serikali ya Zanzibar kiasi cha Sh. bilioni 104 kwa ajili ya mfuko huo ili kuwasaidia kaya maskini.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu wa fedha hizo kila mwaka serikali ya Zanzibar itapewa Sh. milioni 36.7 ili kuendeleza na kuwasaidia wanakaya maskini kujikimu kimaisha.

Alisema kutolewa kwa kiasi kikubwa hicho cha fedha ni kuwathamini wana kaya maskini katika kuimarisha miradi yao na kupunguza umaskini wa kipato.

Alisema katika kipindi hiki cha pili awamu ya tatu TASAF inakusanya kaya zingine ili kunufaika na mfuko huo.

Waziri huyo pia alisema iwapo mawakala wa TASAF watafanya kazi zao kwa uaminifu kutapunguza malalamiko ya wananchi ambao wengine huandikishwa kwa makosa na wengine huwa hawaandikishwi kwa sababu mbalimbali.

Kadhalika, alisema serikali imejipanga kuona kila mwananchi mwenye haki ya kuwamo katika mpango wa kaya maskini anaandikwa ili anufaike na mfuko huo.

“Miradi yote niliyotembelea hapa Zanzibar inayotokana na TASAF ipo vizuri na yakupigiwa mfano ikiwamo hospitali ya Kiyanga kwa kuwapunguzia wananchi masafa ya kutafuta huduma ya afya,” alisema.

Akisoma risala Mjumbe wa Kamati ya Shule ya Fujoni, Ali Haji Abdallah, alisema ujenzi wa jengo hilo ni makubaliano ya wanakijiji ili kuwanufaisha wanafunzi wa shule hiyo na baadaye ukumbusho huo utumike kwa mambo mengine ikiwamo mikutano.

Alisema hivi sasa jengo hilo liko tayari kwa kufunguliwa lianze kutumika katika mambo ya kijamii.

Kwa upande wake Mratibu wa shughuli za serikali, Khalid Bakari Hamrani, alisema jengo hilo limeanza kujengwa kutokana na watoto wa shule hiyo kufanya mitihani yao chini ya miti na wakatafuta kiwanja na kuikabidhi TASAF kwa ujenzi huo.

Alisema awali ujenzi huo ulipangwa kutumia kiasi cha Sh. milioni 98 lakini wakaja na mbinu ya kufanya ukumbi huo kuwa wa kisasa na wenye ubora ukagharimu Sh. milioni 118.



Naibu Spika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, akiwapa sadaka watoto yatima wanaoishi na virusi vya Ukimwi katika kituo cha Zaso Children Home kilichoko Fuoni Mambosasa nje ya Mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwenge wa Uhuru kuzinduliwa Makunduchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENGE wa Uhuru unatarajiwa kuzinduliwa leo huko Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, alisema maandalizi ya uzinduzi wa mbio za Mwenge huo umeshakamilika na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi.

Alisema mwaka jana Mwenge huo ulikuwa uzinduliwe Mkoa wa Kusini, lakini kutokana na Corona ukaahirishwa na ndio ulikuwa mwenyeji wa uzinduzi huo.

Alisema kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo imejipanga ili kuhakikisha kuwa mambo yote yanakuwa salama wakati wote wa uzinduzi wa mbio hizo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mbio hizo mwaka 1964, Mwenge wa Uhuru umekuwa kichocheo kikubwa katika kuhamasisha maendeleo, uzalendo, umoja, mshikamano na kudumisha amani ya Taifa laTanzania.

Alisema kama ilivyo kawaida ya Mwenge wa Uhuru huambatana na uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na mwaka huu kutazinduliwa miradi hiyo ikiwamo ya afya, elimu na miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema baada ya uzinduzi huo utatembezwa katika Wilaya ya Kusini na baadaye kukabidhiwa katika Wilaya ya Kati Unguja kwa kuendelea na mbio zake katika mikoa na wilaya zingine.

Kaulimbiu ya mwaka huu TEHAMA ni msingi wa taifa endelevu, itumie kwa usahihi na uwajibikaji.

# Watendaji watakiwa kukabiliana matukio ya hatari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, amewataka watendaji wa taasisi zinazoshughulikia rasilimali watu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ili kuepukana matukio ya hatari.

Aliyasema hayo jana wakati akikagua Bandari ya Malindi Zanzibar na kuchunguza vyombo vya usafiri vinavyosafirisha abiria.

Alisema kuwa ni vyema wafanyakazi wakapewa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa sababu hawana uelewa wowote maafa yanapotokea.

Aliwataka wafanyakazi wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA), kuweka utaribu mzuri wa usalama wa abiria na mali zao kwa sababu hakuna sehemu ya dharura.

Aliwataka watendaji hao kuweka mpango mzuri wa kushusha abiria na magari ili kuondoa usumbufu kwa wasafiri bandarini.

Pia aliwataka kusimamia vyombo ambavyo havifuati utaratibu uliowekwa na kuvichukulia hatua za kisheria vinapokiuka maagizo wanayopewa.

“Haiwezekani vyombo kupakia abiria kupita kiasi huku wakifukuzana baharini jambo ambalo linahatarisha maisha ya watu na mali zao, tukipoteza rasilimali watu tunapoteza nguvu kazi wa taifa,” alisema.

Alisema lazima kuwapo na mawasiliano na ushirikiano kwa wafanyakazi ili kuwe na mabadiliko kwa lengo la kuziondoa changamoto zilizopo. Alisema kuwa ukaguzi huo umefanyika kwa mujibu wa Sheria namba moja ya mwaka 2015 ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kutoka kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Ukaguzi huo ulishirikisha taasisi mbalimbali zilizomo kwenye mpango kazi wa kukabiliana na maafa ikiwamo kikosi vya ulinzi na usalama, Kikosi Maalum ya Kuzuia Magendo (KMKM) na Kikosi cha Zimamoto.

# Kukosa mwongozo afya kikwazo wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

KUKOSEKANA kwa mwongozo maalumu unaowasimamia watoa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya nchini ni kikwazo kikubwa kwa watu wenye ulemavu (WWU) kupata huduma stahiki.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa watoa huduma za afya kutoka hospitali mbalimbali za jijini Dar es Salaam, yaliyoandaliwa na Chama cha Walimu wenye Uziwi Tanzania (CWUT) na kufadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS).

Akizungumza katika mafunzo hayo, Dk. John Bosco kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili alisema kuna umuhimu wa mwongozo huo utakaotatua masuala ya miundombinu, mawasiliano na mtazamo potofu ili kuwezesha watu wenye ulemavu kupata huduma stahiki.

"Kwa sasa hakuna mwongozo maalumu licha ya ule uliopo kugusia watu wenye ulemavu kwenye baadhi ya maeneo kama vile sera ya afya ya mwaka 2007 na sera ya kujikinga na maambukizi ya Ukimwi," alisema Dk. Bosco.

Pia aliongeza: "Iwapo tutakuja na mwongozo, unaozungumzia huduma za afya kwa watu wenye ulemavu itasaidia sana kupunguza changamoto zilizopo."

Awali mratibu wa mradi huo, Francis Mbisso alisema changamoto hizo ni za miaka mingi pamoja na uwapo wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu, Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2010) na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu ambayo Tanzania iliusaini mwaka 2009.

"Miongoni mwa changamoto hizo ni watoa huduma za afya kutojua lugha ya alama hivyo viziwi hukosa tiba stahiki kwa vile kile kinachomsumbua hakijaeleweka ukizingatia wengi wao hawajui kusoma na kuandika," alisema Mbisso.

"Changamoto hizi ndizo zilizotufanya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuja na mafunzo haya ili kuwezesha huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya mjini Dar es Salaam kuzingatia mahitaji maalum kwa watu wenye ulemavu na kuinua uelewa wa watoa huduma kuhusu sheria na sera zinazolinda haki za afya kwa walemavu," aliongeza Mbisso.




Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa, akisisitiza jambo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya ubunifu jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Bolt ilivyopaisha ajira sekta binafsi

**Na Christina Mwakangale**

MFUMO wa kuagiza usafiri kupitia mtandao, ikiwamo huduma ya Bolt, umeinua ajira kwenye sekta binafsi nchini, kutoka asilimia 9.8 hadi 29.

Happiness Njunwa, mmoja wa madereva waliojiajiri na kutumia mfumo huo, akizungumza mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, alisema anatumia mfumo wa Bolt, kupata wateja ambao hukodisha bajaji kwa safari tofauti.

"Nimefanya kazi ya kuendesha bajaji jijini Dar es Salaam na ni kwa mkataba maalum na mwenye chombo kwa kipindi cha mwaka mmoja sasa, baada ya kukosa ajira za ofisini.

"Mfumo wa kuangiza usafiri kwa njia ya mtandao umetuongezea uhakika wa kupata abiria na kipato, unatusaidia sana kwa maana unatuunganisha moja kwa moja na watu wanaohitaji usafiri, " alisema Happiness.

Kwa mujibu wa ripoti ya Soko la Ajira Tanzania ya mwaka 2018, inaonyesha kuwa takriban asilimia 9.8 ya watu wote wazima hawakuwa na ajira katika kipindi hicho na kwamba Bolt imewezesha maelfu wa madereva, wanaotafuta ajira kupata fursa mpya za kujipatia na kujiongozea kipato.

Meneja wa Bolt Tanzania, Remmy Eseka, alisema madereva waliojiunga na huduma zinazotolewa na mfumo huo, wana uhakika wa kupata kipato kila siku.

"Madereva wanatumia mfumo wa Bolt kuanzisha biashara zao wenyewe na kupata mapato ya uhakika yanayowawezesha kuhudumia familia zao.

"Baadhi ya madereva wanatumia magari na pikipiki zao wenyewe, na wengine wameajiriwa na wamiliki wa vyombo vya moto walioanzisha biashara zao za usafiri," alisema Remmy na kuongeza;

"Tunafurahi kutoa fursa za kazi na za biashara zinazowawezesha watu kujipatia kipato na kuboresha maisha yao. Pia tunafurahi kuwezesha Watanzania wanaoishi Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma kupata usafiri wa uhakika kwa bei nafuu."

# Benki yaungana na Pinda upandaji wa miti 10,000

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imeungana na Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, katika kufanikisha kampeni maalum ya kupanda miti 10,000 katika kata ya Zuzu jijini Dodoma.

Imeelezwa kuwa lengo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhifadhi mazingira.

Jitihada za benki hiyo ni mwendelezo wa mpango mkakati wake wa kutunza mazingira ujulikanao kama 'Exim Go Green Initiative.'

Katika kufanikisha kampeni hiyo iliyoratibiwa na Taasisi ya Habari Development, benki hiyo pia imechangia fedha ili kufanikisha ununuzi wa miti katika zoezi hilo muhimu lililohudhuriwa pia na viongozi waandamizi wa serikali waliojitokeza kuunga mkono jitihada za Pinda.

Baadhi ya viongozi hao ni pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, wafanyakazi wa benki hiyo, walimu na wananchi wa kata hiyo.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Pinda pamoja na kuipongeza Benki ya Exim kwa kufadhili zoezi hilo muhimu, alielezea umuhimu wa kutunza mazingira, huku akibainisha baadhi ya changamoto zitokanazo na uharibu wa mazingira ni ukame na mabadiliko ya tabianchi.

"Ndio maana binafsi nimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba nashirikiana kikamilifu na wadau mbalimbali zikiwamo taasisi kama benki ya Exim ili kwa pamoja tuhakikishe tunaitengeza Tanzania ya kijani," alisema Pinda ambaye alitumia pia wasaa huo kuwatembeza wageni hao kwenye miradi yake mbalimbali ikiwamo ya kilimo na utunzaji wa mazingira.

Mkuu wa kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Stanley Kafu, alisema utunzaji mazingira ni sehemu ya vipaumbele vya benki hiyo na ndio sababu imekuwa mstari wa mbele kubuni na kuunga mkono jitihada mbalimbali za utunzaji mazingira nchini ikiwamo upandaji wa miti na utunzaji wa bustani mbalimbali zilizopo katikati ya miji na majiji mbalimbali hapa nchini.

"Mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa uharibifu wa mazingira yamekuwa na athari kubwa kiuchumi kwa kuwa yamekuwa yakizorotesha pia shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji na ustawi wajamii kwa ujumla. Ni wazi kwamba hatuwezi kutenganisha athari hizi na ufanisi wa biashara za kibenki na hiyo ndio sababu tunashiriki kikamilifu katika kutatua changamoto hii," alifafanua.

Zaidi, aliwasihi wananchi hususani wakazi wa kata ya Zuzu kuzingatia na kuheshimu sheria zinazosimamia na kulinda misitu ili waweze kunufaika na rasilimali hiyo muhimu.

HABARI KIMATAIFA

# Macron mwenyeji mkutano wa uchumi barani Afrika



**Paris,** UFARANSA


RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron (pichani) kesho atakuwa mwenyeji wa mkutano wa kilele wa viongozi wa Ulaya na Afrika katika kutafuta suluhisho la mgogoro wa kifedha wa Afrika.

Mkutano huo wa kilele wa ufadhili wa uchumi wa Afrika, utafanyika kwa njia ya mtandao na kuwakutanisha wakuu wa nchi 30.

Awali, ulikuwa ufanyike mwaka jana baada ya Shirika la Fedha Duniani (IMF), kutabiri kuwa uchumi wa Afrika uko hatarini kuingia katika pengo la kifedha la dola bilioni 290 kufikia mwaka 2023.

Ukuaji uchumi barani Afrika, ambao ulishuhudia anguko lake la kwanza mwaka uliopita, unatarajiwa kuongezeka hadi asiliimia 3.4 mwaka huu na asilimia 4.0 kwa mwaka ujao.

Ucheleweshaji wa ulipaji madeni uliowekwa Aprili mwaka jana na kundi la nchi za G20 na kundi la wakopeshaji wa Paris, uliipa Afrika nafasi ya kupumua, ikisitisha ulipaji wa euro bilioni 5.7. **DW**



Mtoto aliyeokolewa katika kifusi akiwa amebebwa na kijana wa Kipalestina, baada ya nyumba yao kuharibiwa kufuatia mashambulizi ya angani ya Israel, jijini Gaza, jana. Shambulio hilo liliua watu takribani 26. **PICHA: AP**

## UNICEF yasikitika vifo vya watoto 40 Gaza

**Amma,** JORDAN

WATOTO wanane wa kipalestina wameuawa usiku wa kuamkia jana, Ukanda wa Gaza na kufanya idadi ya watoto waliouawa hadi sasa kufikia 40.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), lilisema hayo jana.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, lilikutana jana, kuujadili mgogoro huo kati ya Israel na Palestina. Mkurugenzi wa UNICEF Kanda ya Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini, Ted Chaiban, alinukuliwa kupitia taarifa iliyotolewa jana, mjini Amma, akisema;

"Watoto wanane wa Kipalestina wameuawa Kaskazini mwa Gaza usiku wa kuamkia leo (jana) na kufanya idadi ya watoto waliouawa tangu Mei 10, mwaka huu, kufikia 40."

"Umri wa watoto hao ni kati ya miezi sita hadi miaka 17, na nusu ya hao 40 walikuwa na umri wa chini ya miaka 10."

Chaiban alisema zaidi ya watu 1,000 waliripotiwa kujeruhiwa, wengine wakiwa na majeraha makubwa wakiwamo watoto.

Pia Israel, watoto wawili, akiwamo mwenye umri wa miaka sita waliuawa tangu kuanza kwa mashambulizi kutoka pande zote mbili, siku tano zilizopita.

"Wiki iliyopita, huko Ukingo wa Magharibi wa Mto Jordan, pamoja na Jerusalem Mashariki, mtoto mmoja mwenye umri wa miaka 16 aliuawa na watoto wengine 54 wa Kipalestina walijeruhiwa huku 26 wakikamatwa.

Hata hivyo wengi wao wameshaachiliwa huru," alisema Mkurugenzi huyo wa UNICEF.

Pia alisema, shule 35 katika ukanda wa Gaza ziliharibiwa na nyingine 29 zikitumika kama makazi ya muda, kwa familia ambazo zimekimbia makazi yao kutokana na mashambulizi ya makombora.

Alisema idadi kubwa ya wakimbizi hao wa ndani 10,000 ni watoto na kwamba UNICEF imepokea ripoti kuwa huko Israel shule tatu zimeharibiwa.

Wakati huo huo, nyumba ya kiongozi wa kundi la Hamas, ilipigwa bomu jana na majeshi ya Israel katika Ukanda wa Gaza, huku kundi hilo nalo likiripotiwa kufyatua makombora yaliyoelekezwa katika mji wa Tel Aviv.

Kiongozi huyo Yehya Al-Sinwar, ameliongoza kisiasa na kijeshi kundi la wapiganaji wa Hamas katika Ukanda wa Gaza tangu mwaka 2017. **UN/DW**

## VOA yajivunia miaka 59 kuhabarisha Kiswahili

**Washington,** MAREKANI

IDHAA ya Kiswahili ya Sauti ya Amerika (VOA), imetimiza rasmi miaka 59 tangu kuanzishwa kwa chombo hicho kinachohabarisha kwa lugha hiyo, kilichoanzishwa mwaka 1962.

Idhaa hii ilipoanzishwa ilikuwa na matangazo yaliyokuwa yakirekodiwa na kurushwa baadaye ikiwa na watangazaji wachache.

Kadri miaka inavyokwenda Idhaa hiyo, inajivunia kwa kuwa na idadi kubwa ya wasikilizaji maeneo ya Afrika Mashariki na Kati na matangazo ambayo pia husikika kupitia kwenye tovuti ya voaswahili na mitandao yake ya kijamii pamoja na idadi kubwa ya watangazaji mahiri na wazalishaji.

Idhaa imeendelea kupanuka kwa kuanzisha vipindi vya televisheni ikiwamo Duniani Leo, ambacho kila siku huwa hewani na vingine ni Maisha na Afya, Washington Bureau pamoja na Zulia Jekundu.

Idhaa inalenga matangazo yake kwa msikilizaji wa kila umri kuanzia wazee hadi vijana kupitia lugha ya Kiswahili na kuwapatia vipindi mbalimbali ambavyo vinalenga maisha ya kila siku kuanzia habari za afya, jamii, uchumi, elimu na siasa na hutoa fursa kwa wasikilizaji kutuma maoni na salamu zao.

Idhaa ya Kiswahili iliwasihi wasikilizaji wake kuendelea kusikiliza matangazo hayo kupitia lugha hiyo. **VOA**

## WHO: Corona itakuwa hatari zaidi 2021

**Washington,** MAREKANI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetangaza kuwa janga la Covid-19 litakuwa hatari zaidi mwaka huu, kuliko mwaka jana

WHO, lilisema kwamba mwaka wa 2021 utakuwa mbaya zaidi, kuliko corona iliyoibuka China mwishoni mwa mwaka 2019 na ikageuka kuwa janga kubwa kwa kuenea kote ulimwenguni mnamo 2020.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO Tedros Adhanom Ghebreyesus alisema;

"Tunaamini mwaka wa pili wa janga hili utakuwa mbaya zaidi kuliko ule wa kwanza." Alibainisha kwamba wimbi la pili la janga hilo nchini India limeleta wasiwasi mkubwa. **TRT**

## HABARI MICHEZO



# CHELSEA WATAJIWA DAU LA LUKAKU

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea wameambiwa kuwa wanaweza kumsajili nyota wa Inter Milan, Romelu Lukaku ikiwa tu wataweza kufikia dau linalotajwa na klabu hiyo.

Nyota huyu raia wa Ubelgiji amekuwa na msimu mzuri Inter, akiwa amefunga mabao 28 kwa msimu huu klabuni hapo.

Idadi ya mabao inahusisha 22 ya Serie A, akiwasaidia Inter kupata taji lao la kwanza baada ya miaka 11.

Inter kwa sasa wapo kwenye hali ngumu kiuchumi, hivyo klabu inaweza kulazimika kuachana na wachezaji kadhaa wakubwa kikosini hapo, ili kuweka sawa hali yao ya kiuchumi, wakati baadhi yao wakiombwa kukubali kupunguzwa mshahara.

Kwa mujibu wa Corriere dello Sport, Lukaku ni miongoni mwa wale ambao wanatarajiwa kuathirika na hali hii na anaweza kuondoka ikiwa tu wanaomhitaji watalipa dau la Euro milioni 120.

Chelsea wametajwa kuwa wanaisaka saini ya nyota wao huyo wa zamani, ambaye amewahi kucheza mechi 15 akiwa pale Stamford Bridge.

Manchester City pia wanahusishwa na uhamisho huo licha ya Pep Guardiola kusisitiza kuwa hawatafanya uhamisho wa fedha nyingi.

## Guardiola: Klopp kanifanya niwe bora



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kocha wa Liverpool, Jorgen Klopp, amemfanya azidi kuwa bora kutokana na changamoto anayompa.

Guardiola amesema Klopp amemfanya kila siku awe anafikiria mbinu mpya za kushinda michezo.

Baada ya City kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England, Klopp alimtumia ujumbe wa pongezi.

Baada ya kupokea salamu hizo za pongezi Pep raia wa Hispania amesema; "Ninamthamini sana, yeye na kocha wa Everton, Carlo Ancelotti, wamefanya hivyo.

"Kwa hiyo nawathamini sana wote wawili. Bado sijapata nafasi ya kujibu ujumbe, lakini nitafanya hivyo. "Jurgen, kwa kweli, ni msukumo mkubwa kwangu na amenifanya kuwa bora kupitia timu zake wakati yupo Borussia Dortmund na sasa Liverpool.

"Amenifanya mimi kuwa kocha bora kabisa."

Man City walitangazwa kuwa mabingwa wa Ligi Kuu England msimu huu wa 2020-21 Jumanne baada ya Manchester United kufungwa mabao 2-1 na Leicester City, na kufanya tofauti ya alama kati yao kuwa 10.

## *Hakimi afunguka ya Conte kumvuta Inter Milan*

**MILAN,** Italia

ACHRAF Hakimi amebainisha kuwa Antonio Conte alikuwa na nafasi kubwa sana kumshawishi ajiunge na klabu ya Inter Milan.

Hakimi amesema Conte alimuita na kumfanya ajione mchezaji muhimu na hivyo akakubali kujiunga na mabingwa hao wa Italia.

"Aliniita na kunifanya nijione muhimu," alisema akinukuliwa na Sky Sport Italia.

Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid na Borussia Dortmund, alizungumzia hamasa yake kujiunga na Inter msimu wa majira ya joto uliopita kwa dau la Euro milioni 40.

Hakimi mwenye umri wa miaka 22, alisema Conte alimuita na kumshawishi kuijiunga na klabu hiyo, na kutokana na wito huo alijiona kuwa sehemu muhimu.

Akizungumzia hali ya sasa na kikosi cha Conte, amesema kuwa anadhani ni wakati wao kuanza kushinda Ulaya.

Alisema anajali watu wanaolielewa soka na wanamkubali na kuutambua mchango wake kwa namna anavyocheza.

"Ninachojali ni wale wanaoelewa soka na kukubali namna ninavyocheza. Hapa, nimejifunza namna ya kujilinda vizuri zaidi ya nilivyokuwa mwanzo."



# Arsenal yamkatalia bilionea wa Spotify

**LONDON,** England

OFISA Mtendaji Mkuu wa Spotify, Daniel Ek amedai kuwa ofa yake ya kutaka kuinunua Arsenal imekataliwa wiki hii, lakini amesisitiza bado ana nia ya kuinunua klabu hiyo.

Huku kukiwa na presha kubwa kwa wamiliki Kroenke Sports & Entertainment baada ya kujiingiza kwenye mashindano mapya ya Ulaya, Ek alitangaza kutaka kuinunua klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Ek ambaye ni raia wa Sweden na shabiki wa Arsenal tangu utotoni, aliposti kwenye Twitter yake mwezi uliopita akiandika “ninataka kuinunua Arsenal.”

Magwiji wa ‘Washikabunduki’ hao, Thierry Henry, Patrick Vieira na Dennis Bergkamp wamekuwa wakimuunga mkono bilionea huyo aliyetoa ofa ya pauni bilioni 1.8 kuinunua klabu hiyo.

Henry aliiambia Sky Sports kwamba mchakato wa kuiuza Arsenal utakuwa mrefu na si rahisi na Jumamosi, Ek aliposti kwenye mtandao wake wa kijamii akisema kwamba ofa yake imekataliwa.

“Nataka kuweka wazi kuhusu taarifa ya Arsenal ikisema kwamba sikutoa ofa yoyote,” aliandika Ek.

“Nafikiri ni muhimu kuweka rekodi sawa, nilitoa ofa mapema wiki hii kwa Josh Kroenke na benki yao kuhusu kutaka kuinunua klabu.

“Walijibu kwamba, hawahitaji fedha. Naheshimu maamuzi yao, lakini bado nina nia ya dhati kuinunua klabu hii.”



# VARDY ATAJA MATAJI ZAIDI BAADA YA FA



**LONDON,** England

JAMIE Vardy anaangalia uwezekano wa kuongeza mataji zaidi akiwa na Leicester City baada ya kuwasaidia ‘Mbwa Mwitu’ hao kutwaa taji lao la kwanza la FA.

Leicester, ambao walishinda taji la Ligi Kuu England na Vardy msimu wa 2015-16, hatimaye walilitwaa Kombe la FA baada ya kuifunga Chelsea bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali juzi, Jumamosi.

Youri Tielemans alifunga bao pekee kwa kikosi hicho cha kocha Brendan Rodgers pale katika dimba la Wembley, huku bao la dakika za majeruhi la kujifunga la Wes Morgan likikataliwa na VAR.

Vardy sasa amecheza katika kila raundi ya mashindano hayo ikiwamo hatua ya awali, akiwa ameanza soka kwenye ligi za chini.

Na sasa Vardy anataka kubeba mataji zaidi na Leicester baada ya Kombe hilo la FA.

“Ni hisia za aina yake, kwa hakika kabisa. Hatimaye tumeweza kulitwaa taji hili,” alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

“Lakini miaka miwili iliyopita tuliona kama ni jambo gumu kwetu kulibeba taji kama hili, na leo (juzi) tumeweza na sasa nataka mataji zaidi.”

# *Inter sasa yahaha kumbakiza Conte*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte atakutana na Mwenyekiti wa Inter Milan, Steven Zhang, “haraka iwezekanavyo” wakati mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia wakiangalia kumbakisha kocha huyo hapo San Siro.

Hofu kuhusu matatizo ya kifedha yanayoikumba Inter yameibua uvumi siku za hivi karibuni kwamba, Conte anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Klabu hiyo imewaomba wachezaji wake kukubali kupunguziwa mishahara, huku nyota wake kama Romelu Lukaku na Lautaro Martinez wakiwa wanahusishwa na mpango wa kuondoka.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Inter, Giuseppe Marotta, hivi karibuni alisisitiza kwamba klabu itaheshimu mikataba kama wachezaji watakataa kupunguziwa mishahara. Lakini wakati kukiwa na sintofahamu kuhusu majaliwa ya Conte, Marotta ana matumaini mambo yatakwenda kama yalivyopangwa.

“Yeye ni mshindi na ameonyesha hivyo hapa,” alisema Marotta kuhusu Conte.

Akizungumza na Sky Sport Italia, Marotta alisema: “Haraka iwezekanavyo watakutana na rais, nina matumaini tunaweza kuendelea.”



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI ATAKIWA KUMRITHI MBAPPE PSG

●●● Matajiri hao wa jijini Paris wapo tayari kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili...

**PARIS,** Ufaransa

JARIDA la L'Equipe limedai kwamba, klabu ya Paris Saint-Germain imemweka straika wa Bayern Munich, Robert Lewandowski kuwa kipaumbele chao katika dirisha la usajili kama Kylian Mbappe ataondoka.

**Majaliwa ya Mbappe bado hayajulikani katika klabu hiyo huku akitajwa kama anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu.**

Na sasa matajiri hao wa jijini Paris wapo tayari kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kutafuta mbadala wa Mbappe mwenye umri wa miaka 22.

PSG ambao kwa sasa wapo kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, walitolewa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Manchester City.

Mbappe amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kuhamia kwa miamba wa Hispania, Real Madrid pamoja na Liverpool na Manchester United. Kwa mujibu wa ripoti ya L'Equipe, PSG wanaona kwamba Lewandowski ndiye chaguo sahihi kwa usajili wao wa majira ya joto.

Nyota huyo wa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ambaye juzi, Jumamosi aliifikia rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao mengi zaidi (40) kwenye ligi hiyo kwa msimu mmoja, pia amekuwa akihusishwa na kutaka kwenda Ligi Kuu England.

Lewandowski alifunga kwa penalti wakati Bayern ikitoka sare ya 2-2 dhidi ya Freiburg na kufikisha mabao 40 aliyofunga msimu huu na kuifikia rekodi ya Muller.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland anaweza kuweka rekodi mpya kwa sababu bado Bayern ina mchezo mmoja kumaliza ligi msimu huu.

Lewandowski mkataba wake wa sasa na Bayern unamalizika mwaka 2023.

## ZISIKUPITE

### ZIDANE KUONDOKA MADRID

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amekiambia kikosi chake kwamba, ataondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Goal)***

### MESSI APELEKWA MAN CITY

MANCHESTER City imeambiwa inaweza kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, kutoka Barcelona kama wanaweza kumlipa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki baada ya kodi. ***(Sun on Sunday)***

### POGBA ATAKIWA KUSAINI

MANCHESTER United inataka kiungo wake, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, kusaini mkataba mpya, lakini wanamhofia wakala wake Mino Raiola. ***(Sunday Mirror)***

### ARSENAL YAMTAKA BERTRAND

ARSENAL ina matumaini ya kuipiku Manchester City kumsajili mlinzi wa kushoto wa England, Ryan Bertrand mwenye umri wa miaka 31, ambaye ataondoka Southampton mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail on Sunday)***

### HOLGATE KUMPISHA KOULIBALY

EVERTON inajiandaa kumuuza mlinzi wake, Mason Holgate mwenye umri wa miaka 24, ili kupata fedha za kumsajili beki wa kati wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29 kutoka Napoli. ***(Football Insider)***

### DEPAY ANUKIA BARCELONA

STRAIKA wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 27, amewasha taa ya kijani kujiunga na Barcelona. ***(L'Equipe)***

### LIVERPOOL YAMTOSA KABAK

LIVERPOOL haitamsajili mlinzi wa kati wa Uturuki, Ozan Kabak kwa mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alijiunga na timu hiyo kwa mkopo akitokea Schalke, Februari. ***(Sun on Sunday)***

### WATAJWA KUMRITHI ZIDANE

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti na kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, ni miongoni mwa wanaofikiria kumrithi Zinedine Zidane kama akiondoka Real Madrid. ***(Sunday Mirror)***

### KOEMAN AKUTANA NA RAIS

KOCHA ambaye amekalia kuti kavu pale Barcelona, Ronald Koeman amekutana na Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta na amesemwa watazungumza tena mwishoni mwa msimu huu. ***(Goal)***

### ROBERTS AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle inamfuatilia mshambuliaji wa Leeds United na Wales, Tyler Roberts mwenye umri wa miaka 22. ***(Football Insider)***

# WASHINDI WA JOHNNIE WALKER GOFU WAKABIDHIWA ZAWADI

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya mchezo wa gofu maarufu kama TM Cross Country Golf Challenge, yamemalizika jana katika viwanja vya gofu vya Lugalo, Dar es Salaam kwa hafla ya washindi kukabidhiwa zawadi za vikombe.

**Mashindano hayo ambayo yanafanyika kwa mwaka wa nne, yamefadhiliwa na kinywaji cha Johnnie Walker kinachosambazwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) na yaliweza kuwaleta pamoja wachezaji wa gofu wa madaraja mbalimbali.**

Jumla ya washindi 13 wa madaraja tofauti waliondoka na vikombe baada ya kuibuka vinara.

Akizungumzia kuhusu mashindano hayo ambayo huhusisha kucheza kwenye viwanja mashimo tisa badala ya 18, mwazilishe wake, Terence Mwakaliku, alisema mashindano hayo hutoa fursa kwa wachezaji wa gofu kucheza mchezo huo kwa namna ya tofauti na walivyozoea.

"Badala ya kucheza kiwanja kimoja baada ya kingine, mashindano haya yanahusisha kuchanganya viwanja na mashimo pia na hivyo kumfanya mchezaji kupata uzoefu wa tofauti," alisema Mwakaliku.

Mwakaliku aliishukuru Johnnie Walker kwa kufadhli mashindano hayo na kuongeza kuwa udhamini umesaidia kuboresha mashindano na pia kuwavutia wachezaji wengi zaidi kushiriki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti, Mark Ocitti, ambao ni wadhamini wakuu wa mashindano hayo kupitia Johnnie Walker, alisema kinywaji hicho kinajivunia kuwa sehemu ya mashindano hayo ya aina yake.

"Katika mashindano haya kinachofanyika ni kubadilisha uwanja wa kuchezea gofu ili tuweze kucheza kwa namna tofauti na tulivyozoea na hivyo kufurahia kucheza kwa namna tofauti kabisa. Kinywaji chetu cha Johnnie Walker kinatoa ladha pamoja na uzoefu tofauti kwa watumiaji na tuna furahi kudhamini mashindano haya," alisema.

Johnnie Walker ni moja kati pombe kali zenye ubora wa hali ya juu na hadhi ya kimataifa. Kinywaji hiki kina jumla ya aina tano ambazo zimeshinda tuzo za ubora wa kimataifa. Aina hizo ni pamoja na JW Red Label, JW Black Label, JW Green Label, JW Gold Label, na JW Blue Label kila moja ikiwa na historia yake ya kipekee.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (kushoto), akimkabidhi kikombe mshindi wa Daraja C katika mashindano ya Johnnie Walker TM Cross County Challenge 2021, Danstan Kolimba, baada ya kuibuka mshindi katika viwanja vya gofu Lugalo. Wa pili kushoto ni mwanzilishi wa mashindano hayo, Terence Mwakaliku na kulia ni James Mwambona kutoa Simba Courier ambao ni mdhamini mwenza wa mashindano hayo. **MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Gwambina atua Mtibwa Sugar

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar umemnasa aliyekuwa Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Mohammed Badru, ambaye sasa anachukuwa mikoba ya Thierry Hitimana aliyeachana na kikosi cha 'Wakata Miwa' hao wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jijini jana kutoka ndani ya uongozi wa Mtibwa Sugar, zimeeleza kuwa tayari Badru amewasili Morogoro na kufanya mazungumzo na uongozi wa Wakata Miwa hao na kukubaliana leo, atasaini mkataba wa mwaka mmoja kukinoa kikosi hicho.

Taarifa hizo zilieleza kuwa baada ya makubaliano ya pande zote mbili, kocha huyo amekubali kuanza kazi mapema ya kukinoa kikosi hicho kwa kutumia taaluma na mbinu zake kukinusuru na janga la kushuka daraja.

"Ni kweli Badru amefika Morogoro na kila kitu kimeenda vizuri na baada ya mazungumzo jana (juzi), aliende uwanjani (Jamhuri) na kushuhudia timu yetu ikicheza dhidi ya Tanzania Prisons," alisema mtoa habari huyo.

Alisema Badru atapewa jukumu la kutafuta msaidizi wake baada ya uongozi kumwondoa Kocha wao Msaidizi, Vicente Barnabas na kupelekwa katika majukumu mengine.

Kwa upande wa kocha huyo, alisema kwa sasa hawezi kuzungumza lolote kwani anasubiri muda utakapowadia kila kitu kitawekwa wazi na uongozi wa klabu hiyo.

"Ni kweli siko Mwanza kuhusu taarifa za Mtibwa Sugar naomba tusubiri muda utakapofika, kikubwa kazi yangu iniruhusu kwenda kufundisha timu yoyote hapa nchini, ninachoangalia ni maslahi kwa pande zote mbili," alisema Badru.

Alipotafutwa msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alithibitisha kuwapo kwa mazungumzo na kocha huyo na kudai kwamba yuko njiani na muda wowote anaweza kuanza majukumu ya kukinoa kikosi cha timu hiyo.

"Ni kweli kuna mazungumzo na kocha mpya ambaye atakuja kurithi mikoba ya Hitimana, hii ni baada ya kuhakikisha timu yetu inafanikiwa kufanya vizuri katika michezo yetu iliyobaki na kuweza kubaki katika ligi," alisema Kifaru.

## Mwamnyeto: Bado ubingwa upo Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema bado wanamatumaini ya kutwaa ubingwa licha ya kutoka suluhu bila kufungana dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Mwamnyeto alisema hawajakata tamaa na wanahitaji kupambana hadi mwisho wa ligi ndipo watakapojua nafasi halisi ambayo wapo.

"Mechi ilikuwa ngumu sana. Tulitaka kushinda, lakini kwa bahati mbaya tumetoka suluhu, unajua unaweza kupanga hili, Mungu naye anapanga lake. Hatujakata tamaa sisi tunazidi kupambana tu," alisema.

Kwenye mechi yao dhidi ya Namungo, beki huyo wa zamani wa Coastal Union alisema walicheza vema sana, lakini tatizo kubwa aliloliona ilikuwa kwenye ufungaji tu.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Suleiman 'Morocco' alisema walitengeneza nafasi nyingi zaidi kuliko Yanga, lakini walishindwa kuzitumia.

## Geita Gold yatinga Ligi Kuu Bara kibabe

**Na Adam Fungamwango**


BAADA ya misimu miwili kushindwa kupanda Ligi Kuu kwa kufungwa mechi ya mchujo 'play off', hatimaye timu ya Geita Gold ya mkoani Geita imefanikiwa kutinga Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, kwa kuichapa Fountain Gate mabao 2-0 kwenye Uwanja wa CCM Gairo mkoani Morogoro juzi.

Alikuwa ni mchezaji wa zamani wa Mbao FC na Kagera Sugar, Venance Ludovic, aliyepachika mabao yote mawili dakika ya 20 kwa mkwaju wa penalti na dakika ya 37 yaliyoifanya timu hiyo kutinga Ligi Kuu kutoka Kundi B, ikiungana na Mbeya Kwanza ambayo hivi karibuni ilipanda, ikitokea Kundi A.

Gaita imepanda Ligi Kuu baada ya kujikusanyia pointi 37 baada ya kumalizika kwa mechi zote 16, huku washindani wao wa karibu kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, Pamba FC ya Mwanza ikimaliza ikiwa na pointi 36.

# Michezo

Jumatatu Mei 17, 2021
Nipashe



Lewandowski atakiwa kumrithi Mbappe UKURASA 22

HAIKUWA RAHISI...



Mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu, akijaribu kufunga bila mafanikio baada ya beki wa Kaizer Chiefs kuwahi kuucheza mpira kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa FNB, Afrika Kusini juzi. Simba iliambulia kichapo cha mabao 4-0. **MPIGAPICHA WETU**

# *Simba: Tutapindua meza kwa Mkapa*

●●● Yajivunia rekodi kuwabeba, wakumbusha ya Mufulira Wanderers, Mo Dewji, Gomes wasema...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya baadhi ya mashabiki na wadau wa soka kuamini itakuwa vigumu kwa Simba kuweza kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kukubali kipigo cha mabao 4-0 ugenini Afrika Kusini dhidi ya Kaizer Chiefs, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Gomes na uongozi mzima umesema hakuna lisilowezekana.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa FNB, licha ya Simba kumiliki mpira kwa asilimia 65 dhidi ya 35 za wenyeji wao, safu yao ya ulinzi ililazimishwa kufanya makosa yaliyowasababishia kupata kipigo hicho kikubwa kwao tangu kuanza kwa msimu huu.**

Na wakati huu timu hizo zikitarajiwa kurudiana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Jumamosi wiki hii, Gomes amesema hakuna kisichowezekana duniani.

"Hakuna kitu kisichowezekana duniani. Tunaweza kupindua matokeo, mpira hautabiriki. Hata hivyo hatukucheza vibaya," Kocha huyo raia wa Ufaransa alisema.

Akifafanua zaidi alisema: "Tokea mwanzo tulijua tuna mechi ngumu, tuliadhibiwa kwa udhaifu wa mipira ya juu. Hatukuwa imara kuzuia na Kaizer Chiefs walikuwa wazuri mno kushambulia."

Wakati Gomes akieleza hayo, ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez, yeye alikumbushia rekodi ya Simba kupindua matokeo kuwa si nyumbani tu bali hata ikiwa ugenini kama ilivyofanya mwaka 1979 kwenye michuano hiyo dhidi ya Mufulira Wanderers FC ya Zambia.

"Mwaka 1979 tulifungwa nyumbani 0-4 na Mufulira Wanderers ya Zambia, halafu tulipindua kwao kwa ushindi wa 5-0! Chochote kinawezekana. Tusikate tamaa Wanasimba," aliandika katika mtandao wake wa Instagram.

Kwa upande wa Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mahamed "Mo" Dewji, kupitia mtandao wake wa Twitter, yeye aliandika: "Tumepoteza vita, lakini si uwanja wa mapambano. Tutaendelea kupigana kwa damu yetu, jasho na machozi kuishi siku nyingine."

Lakini Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, yeye alisema atakuwa mtu wa mwisho kuamini kwamba kikosi hicho kimeshatolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Simba hii itakwenda kuishangaza Afrika na dunia, tutarudi nyumbani kwa kishindo kikuu na mshtuko mkubwa utakuwa kwenu mnaotubeza sasa, jiandaeni kisaikolojia mapema. Simba itafuzu kwenda nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Inshaallah!"

Kwa matokeo hayo, Simba sasa inapaswa kushinda mabao 5-0 ili kuweza kutinga nusu fainali ambapo mshindi wa jumla atakutana na mshindi kati ya Wydad Casablaca ya Morocco au MC Alger ya Algeria ambayo katika mchezo wa kwanza ikiwa nyumbani ililazimishwa sare ya bao 1-1.

## Yanga sasa msuli kwa JKT Tanzania

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuambulia pointi moja dhidi ya Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara, uongozi wa Yanga umesema sasa unaenda kupambana kutafuta matokeo chanya kwenye mechi yao dhidi ya JKT Tanzania.

Kikosi cha Yanga baada ya mechi hiyo iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoa Lindi, kiliondoka kuelekea Mtwara kukwea 'pipa' kwa safari ya kurejea Dar es Salaam ili kujiandaa kwenda Dodoma kuivaa JKT Tanzania, keshokutwa, Jumatano.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa Yanga, Thabit Kandoro, alisema baada ya mechi hiyo wanakwenda Dodoma kwa kupambania pointi tatu katika mechi hiyo.

Alisema kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi (pichani chini), ameona upungufu katika kikosi chake na sasa anafanyia kazi ili kuweza kupata matokeo chanya katika mechi hiyo ijayo.

"Tumepata pointi moja dhidi ya Namungo FC, ilikuwa mechi ya ushindani, tunashukuru kwa matokeo hayo, sasa kikosi kinaenda Dodoma kujiandaa na dhidi ya JKT Tanzania, Ni mechi ngumu lakini tumejipanga kutafuta matokeo chanya ili kufikia malengo yetu," alisema Kandoro.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >